

# القرآن الحكيم

## QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by

Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy  
(Former Chief Kadhi of  
Zanzibar & Kenya)

21. "Wafuateni hawa wanaokufundisheni bila ya kutaka ujira; na hali ya kuwa wenyewe wameongoka."

22. (Wakamwambia "Kwani wewe umewafuata?") Akasema: "Kwa nini nisimuabudu yule aliyeniumba (na kukuumbeni nyinyi pia) na kwake mtarejeshwa?"

23. "Je, niishike miungu mengine badala yake? Na kama Mwenyezi Mungu akipenda kunidhuru, uombezi wao hautanifaa kitu, wala hawatanioko!"

24. "Nikifanya hivyo nitakuwamo katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri."

25. "Bila shaka mimi nimemuamini Mola wenu (huyo ninayekuambieni), basi nisikilizeni, (na nyinyi mumuamini." Hawakusikiliza maneno yake, bali walimuua.)

26. Akaambiwa "Ingia Peponi." Akasema: "Laiti watu wangu wangejua (haya niliyoyapata wakapata nao kusilimu)"

27. "(Wangejua) jinsi Mola wangu alivyonisamehe na akanijaalia miongoni mwa waliohishimiwa."

28. Na hatukuwateremshia watu wake jeshi kutoka mbinguni (kuwaangamiza) baada yake; wala hatukuwa wateremshao (majeshi mbinguni kwa ajili ya kuangamiza. Malaika mmoja tu anatosha).

29. Basi hakukuwa (kuangamizwa kwao) ila kwa ukelele mmoja tu (uliopigwa na Jibrili); na mara wakawa waliozimika, (Waliokufa)!

30. Inafaa kusikitikiwa hawa waja (wa Mwenyezi Mungu): hakuwajia Mtume yoyote ila walikuwa wanamfanyia mzaha (na wanakataa kumfuata)!

31. Je, hawaoni uma ngapi tuliziangamiza kabla yao? (Hawaoni) kuwa hawarejei kwao?

32. Na hapaza (viumbe) wowote ila watahudhurishwa mbele yetu.

33. Na alama (ya kuonyesha moja ya rehema za Mwenyezi Mungu) juu yao ni ardhi iliyokufa: Tunaifufua na tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila.

34. Na tukafanya ndani yake mabustani ya mitende na mizabibu na kupitisha chemchem ndani yake

اَتَّبِعُوا مَنْ لَا يَسْأَلُكُمْ أَجْرًا وَهُمْ مُهْتَدُونَ ﴿١٠﴾

وَمَا لِيَ لَا أَعْبُدَ الَّذِي فَطَرَنِي وَالَّذِي  
سَرَّبَعُون ﴿١١﴾

أَتَّخِذُ مِنْ دُونِهِ إِلَهًا إِنْ يُرِيدِ الرَّحْمَنُ بِضُرٍّ لَا  
تُغْنِي عَنِّي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا وَلَا يُنْقِذُون ﴿١٢﴾  
إِنِّي إِذَا لَبَّيْتُ صَلَّيْتُ مَيْمِينَ ﴿١٣﴾

إِنِّي آمَنْتُ بِرَبِّكُمْ فَاسْمَعُون ﴿١٤﴾

فَبِئْسَ أَذْخُلُ الْجَنَّةَ قَالَ لَيْتَ قَوْمِي يَعْلَمُونَ ﴿١٥﴾

بِمَا عَفَرْتُ رَأْيِي وَجَعَلْتَنِي مِنَ الْمَكْرَمِينَ ﴿١٦﴾

وَمَا أُنزِلْنَا عَلَى قَوْمِهِ مِنْ بَعْدِهِ مِنْ جُنْدٍ مِنَ  
السَّمَاءِ وَمَا كُنَّا مُنْزِلِينَ ﴿١٧﴾

إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ خَامِدُونَ ﴿١٨﴾

يُحَسِّرُهُ عَلَى الْعِبَادَةِ مَا يَأْتِيهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا  
كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿١٩﴾

أَلَمْ يَرَوْا كَمَا أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنَ الْقُرُونِ أَنَّهُمْ إِلَيْهِمْ لَا  
يَرْجِعُونَ ﴿٢٠﴾

وَإِنْ كُلُّ لُجَّتٍ لَدَيْنَا مُخْضَرَةٌ ﴿٢١﴾

وَأَيُّ لَهُمُ الْأَرْضُ الْمَيْتَةُ أَحْيَيْنَاهَا وَأَخْرَجْنَا  
مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُونَ ﴿٢٢﴾

وَجَعَلْنَا فِيهَا جَنَّاتٍ مِنْ نَجِيلٍ وَأَعْنَابٍ وَوَجَّرْنَا  
فِيهَا مِنَ الْعُيُونِ ﴿٢٣﴾

35. Ili wale katika matunda yake; na haikuyafanya (matunda) hayo mikono yao; je, hawashukuru?

36. Ametukuka Mwenyezi Mungu aliyeumba dume na jike katika (vitu) vyote; katika vile iviotes hayo ardhi, na katika nafsi zao (wanaadamu), na katika vile wasivyovijua.

37. Na usiku ni alama kwao (vile vile ya neema za Mwenyezi Mungu juu ya viumbe vyake); tunauvua humo mchana; mara wao wanakuwa kizani

38. Na jua (pia ni alama kwao); linakwenda (maisha) mpaka kituoni pake. Hayo ni matengenezo ya (Mwenyezi Mungu) Mwenye nguvu (na) Mwenye kujua.

39. Na mwezi (kadhalika ni alama kwao); Tumeupimia vituo, (hiki baada ya hiki); mpaka unakuwa (mwembamba) kama chaparare la mtende kuukuu (lililonywea).

40. Haliwi jua kuufikia mwezi, (wakati wa nguvu zake) wala usiku kuupita mchana, (ukaja kwa ghafla kabla ya wakati wake). Na vyote vinaogelea katika njia (zao)

41. Na ni alama kwao (vile vile ya kuonyesha neema zetu juu yao) kuwa tuliwachukua wazee wao katika majahazi yaliyoshehenewa

42. Na tukawaumbia (viumbe waliokuja baada yao na wanaozidi kuja; tumewaumbia) vipando mfano wa (majahazi, lakini vilivyo vizuri zaidi na vya raha zaidi, kama hizi meli) watakvovipanda.

43. Na kama tukitaka tutawagharikisha (juu ya kuwa vyombo hivi ni madhubuti sana) wala hatakuwako wa kuwasaidia, wala hawataokolewa (maadamu hatutaki)

44. Ila kwa rehema zitokazo kwetu na kuwanufaisha kwa muda kidogo (tu hivi).

يَا كَلِمَاتٍ لَّوْا مِنْ ثَمَرِهِمْ وَمَا عَمِلَتْهُ أَيْدِيهِمْ أَفَلَا يَشْكُرُونَ ﴿٣٥﴾

سَبَّحَنَ الَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا مِمَّا تُثْبِتُ الْأَرْضُ  
وَمِنْ أَنْفُسِهِمْ وَمِمَّا لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾

وَأَيَّةٌ لَهُمُ اللَّيْلُ تَسْكُرُ مِنْهُ النَّهَارُ فَآذَاهُمْ  
مُظْلِمُونَ ﴿٣٧﴾

وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ  
الْعَلِيمِ ﴿٣٨﴾

وَالْقَمَرَ قَدَرْتَهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ  
الْقَدِيمِ ﴿٣٩﴾

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ  
النَّهَارِ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٤٠﴾

وَأَيَّةٌ لَهُمْ أَنَّا حَمَلْنَا ذُرِّيَّتَهُمْ فِي الْفُلْكِ  
الْمَشْحُونِ ﴿٤١﴾

وَخَلَقْنَا لَهُمْ مِنْ مِثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ ﴿٤٢﴾

وَأَنْ لَوْ نَشَاءُ لَنُفِرِّقَهُمْ فَلا صَرِيحَ لَهُمْ وَلَا هُمْ  
يُقَدَّرُونَ ﴿٤٣﴾

إِلَّا رَحْمَةً مِنَّا وَمَتَاعًا إِلَىٰ حِينٍ ﴿٤٤﴾

36. Ndiyo kwanza sasa watalaamu wa ulimwengu wamejua kuwa kumbe hata katika visivyokuwa na roho kuna madume na majike, na kwa mchanganyiko wao ndipo vinapopatikana vinavyopatikana. Na Qurani imetaja haya zamani, na Mwenyezi Mungu akasema humo katika Aya ya 53 ya *Surat Ha Mym Sajdah*, kuwa "Tutawaonyesha (ukweli wa) maneno yetu katika pande zote za ulimwengu, na katika nafsi zao wenyewe, mpaka iwabainikie kuwa haya (yanayosemwa na Qurani) ndiyo haki." Basi Qurani ndicho kitabu cha haki kisichokuwa na upogo wala kosa hata chembe.

42. Huu ukweli mwingine wa Qurani Kiasi cha miaka alfeni imebashiri kuja meli na manuware na masabmarini na motaboti na vyinginevyo vya kwenda baharini. Na ikabashiri kwa kuja mareli, (magari ya moshi) na mamotakari na mabaiskeli na mabasi na maaropleni na mengineyo katika Aya ya 8 ya *Suratun Nahl*. Na ikabashiri pia Qurani kwenda mbinguni — kama wanavyojitahidi watu sasa kutaka kufanya. Mahala pamoja katika ilipoyabaini haya ni katika Aya ya 13 ya *Suratul Jaathiya*.

45. Na wanapoambiwa: “Ogopeni yaliyoko mbele yenu na yaliyoko nyuma yenu mupate kurehemewa;” (hawasikii).

46. Na haiwajii Ishara yoyote katika Ishara za Mola wao (za kuonyesha kuwapo kwake na upweke wake) ila huwa wenye kuipuzza.

47. Na wanapoambiwa: “Toeni katika yale aliyokupeni Mwenyezi Mungu” (msaidie masikini) wale waliokufuru huwaambia walioamini (kwa stihzai): “Je, tuwalishe (tuwaruzuku) ambao Mungu angependa angewalisha yeye Mwenyewe? (Lakini Mwenyewe Mwenyezi Mungu amependa wawe mafakiri, kwa kuwaacha vivyo hivyo bila ya kuwatajirisha). Nyinyi hamumo ila katika upotofu (upotevu) uliyo dhahiri.”

48. Na wanasema: “Abadi hii (ya kuja Kiama) itatokea lini, ikiwa mnasema kweli?”

49. Hawangojei ila ukelele mmoja tu utakaowatoa roho zao, na hali ya kuwa wamo katika hali ya kugombana; (na wengine wamo katika hali nyingine. Muradi kitawajia ghafla).

50. Na hawataweza kuusia (wakati huo) wala hawataweza kurejea kwa watu wao.

51. Na kisha litapigwa baragumu (la kufufuliwa), tahamaki hao wanatoka makaburini kwenda mbiombio kwa Mola wao.

52. (Na huku) wanasema. “Ole wetu, (Ee adhabu yetu)! Nani aliyetufufua malaloni petu?” (Waambiwe): “Haya ndiyo yale aliyoahidi (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema na waliyoyasema kwa haki Mitume.”

53. Haitakuwa ila ukelele mmoja tu, tahamaki wote wamehudhurishwa mbele yetu.

54. (Waambiwe:) “Basi leo nafsi yoyote haitadhulumiwa chochote kile wala hamtalipwa ila yale mliyokuwa mkiyatenda.”

55. “Kwa yakini watu wa Peponi leo wamo katika shughuli (zao), wamefurahi:”

56. Wao na wake zao wamo katika vivuli, wameegemea juu ya viti vya fahari.

57. Watapata humo (kila namna ya) matunda na watapata kila watakavyovitaka.

58. Salama (tu juu yao), ndilo neno litokalo kwa Mola (wao) Mwenye rehema.

وَلَا ذَا قَيْلٍ لَهُمْ أَنْقُوا مَا بَيْنَ أَيْدِيكُمْ وَمَا خَلْفَكُمْ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٥٥﴾

وَمَا تَأْتِيهِمْ مِنْ آيَةٍ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِمْ إِلَّا كَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ ﴿٥٦﴾

وَلَا ذَا قَيْلٍ لَهُمْ أَنْقُوا مَا رَزَقْنَاكُمْ اللَّهُ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَالَّذِينَ آمَنُوا أَنْظِعْهُمَنْ لَوْ يَشَاءُ اللَّهُ أَطَعْتَهُ لَئِنْ أُنزِلَتْ إِلَّا فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٥٧﴾

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٥٨﴾

مَا يَنْظُرُونَ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً تَأْخُذُهُمْ وَهُمْ يَخِصِّمُونَ ﴿٥٩﴾

فَلَا يَسْتَطِيعُونَ تَوْصِيَةً وَلَا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ يَرْجِعُونَ ﴿٦٠﴾

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَأَذا هُمْ مِنَ الْأَجْدَاثِ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يَنْسِلُونَ ﴿٦١﴾

قَالُوا يَا بَوِئسنا مَن بَعَدنا مِنْ مَرْقَدنا يَءِ هَذا ما وَعَدَ الرَّحْمَنُ وَصَدَقَ الْمَرْسُلُونَ ﴿٦٢﴾

إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَأَذا هُمْ جَمِيعٌ لَدَيْنا مُخْضَرُونَ ﴿٦٣﴾

قَالِيَوْمَ لَا تُظَلَمُ نَفْسٌ شَيْئاً وَلَا تُجْزَوْنَ إِلَّا ما كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٤﴾

إِنَّ أَصْحابَ الْجَنَّةِ الْيَوْمَ فِي شُغُلٍ فَاكُهُونَ ﴿٦٥﴾

هُم وَأَزْواجُهُمْ فِي ظِلِّلٍ عَلَى الْأَرْياكِ مُتَكِيُونَ ﴿٦٦﴾

لَهُمْ فِيها فاكهةٌ وَلَهُمْ ما يَدْعُونَ ﴿٦٧﴾

سَلَامٌ قَوْلًا مِنْ رَبِّ رَحِيمٍ ﴿٦٨﴾

59. Na (Wabaya wataambiwa): "Jitengeni leo enyi wabaya"!

60. "Je, sikukuagizeni (sikukuusieni) enyi wanaadamu kuwa msimuabudu Shetani? Hakika yeye ni adui aliye dhahiri kwenu"

61. Na ya kwamba niabuduni mimi. Hii ndiyo njia iliyonyoka.

62. "Na bila shaka aliwapoteza viumbe wengi (kabisa) miongoni mwenu: je, hamkuwa mkifikiri?"

63. "Basi hii ndiyo Jahanamu mliyokuwa mkiahidiwa."

64. "Ingieni leo kwa sababu ya ukafiri wenu."

65. Siku hiyo tutaviziba vinywa vyao, ituzungumze mikono yao na itoe ushahidi miguu yao kwa yale waliyokuwa wakiyachuma.

66. Na kama tungependa tungewapofoa macho yao; wakawa wanakimbilia njia; lakini wangeonaje?

67. Na kama tungetaka tungewafanya (wakawa) vinyama papo hapo mahala pao (walipokaa), basi wasingeweza kwenda wala kurudi.

68. Na tunayempa umri (mrefu) tunamrejea nyuma katika umbo (lake). (Anakuwa kama mtoto). Basi je, hawayatii akilini (haya)?

69. Wala hatukumfundisha (Muhammad) mashairi, wala haiwi kwake (kuwa mtunga mashairi). Haikuwa (Qurani) ila ni ukumbusho na kitabu kibainishacho (kila yanayohitajiwa)

70. Ili amwonye aliye hai na ihakikike kauli (ya kuadhibiwa), juu ya makafiri.

71. Je, hawaoni ya kwamba tumewaambia, katika vile ilivyovifanya mikono yetu (Tumewaambia) wanyama hawa wanaowamiliki.

72. Na tumewatiishia (wanyama) hao, basi baadhi yao wanawapanda na wengine wao wanawala.

73. Na katika hao wanapata manufaa (mengi mengineyo) na vinywaji (vya kila namna). Basi je, hawashukuru?

وَاصْتَارُوا الْيَوْمَ أَيُّهَا الْمُجْرِمُونَ ﴿٥٩﴾

أَلَمْ نَحْمَدْ إِلَيْكُمْ يَوْمَ آدَمَ أَنْ لَا تَعْبُدُوا الشَّيْطَانَ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٦٠﴾

وَأَنْ أَعْبُدُونِي هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾

وَلَقَدْ أَضَلُّ مِنْكُمْ جِبِلًّا كَثِيرًا أَفَلَمْ تَكُونُوا تَعْقِلُونَ ﴿٦٢﴾

هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٦٣﴾

إِصْرُوهَا الْيَوْمَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٦٤﴾

الْيَوْمَ نَخْتِمُ عَلَىٰ أَفْوَاهِهِمْ وَتُكَلِّمُنَا أَيْدِيهِمْ وَنَشْهَدُ أَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٦٥﴾

وَلَوْ نَشَاءُ لَطَمَسْنَا عَلَىٰ أَعْيُنِهِمْ فَاسْتَبَقُوا الصِّرَاطَ فَأَنَّى يُبْصِرُونَ ﴿٦٦﴾

وَلَوْ نَشَاءُ لَسَخْنَاهُمْ عَلَىٰ مَكَانَتِهِمْ فَمَا اسْتَطَاعُوا مُضِيًّا وَلَا يَرْجِعُونَ ﴿٦٧﴾

وَمَنْ يَعْصِرْهُ نُكَّسَهُ فِي الْخَلْقِ أَفَلَا يَعْقِلُونَ ﴿٦٨﴾

وَمَا عَلَّمْنَاهُ الشُّعْرَ وَمَا يَنْبَغُ لَهُ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ وَقُرْآنٌ مُبِينٌ ﴿٦٩﴾

لِيُنذِرَ مَنْ كَانَ كَافِرًا وَيُحِقَّ الْقَوْلَ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٧٠﴾

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا خَلَقْنَا لَهُمْ مِنَّا عَمَلَتْ أَيْدِيَنَا أَنْعَامًا فَهُمْ لَهَا مَالِكُونَ ﴿٧١﴾

وَذَلَّلْنَاهَا لَهُمْ فَمِنْهَا رَكُوبُهُمْ وَمِنْهَا يَأْكُلُونَ ﴿٧٢﴾

وَلَهُمْ فِيهَا مَنَاقِفُ وَمَسَارِبٌ أَفَلَا يَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾

68. Katika Aya hii waliyoifanya ya 69 wamejitia tena kupachika waliyopachika ili wakatae kurejea kwa Nabii Isa mwisho wa ulimwengu, ambavyo ndivyo alivyotwambia Mtume, kama tulivyobaini katika marejezo ya Aya 55 ya Surat Aali Imran.

74. Na wameishika miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili wapate kusaidiwa nao!

75. (Lakini) hawawezi kuwasaidia. Kee wao hao (wanaowaabudu) ndio wanaokuwa maaskari wanaohudhurishwa (kuwalinda masanamu hao)!

76. Basi yasikuhuzunishe maneno yao (wanayokutukania), bila shaka sisi tunajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza.

77. Je, mwanaadamu hatambui ya kwamba tumemuumba kwa tone la manii? Amekuwa hasimu yetu aliye dhahiri (Sasa)!

78. Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake (kwa manii) — akasema: “Nani atakayeihisha mifupa na hali imesagika?”

79. Sema: “Ataihuisha yule aliyeiumba mara ya kwanza, naye ni Mjuzi wa kila (namna ya) kuumba ”

80. Ambaye amekufanyieni moto katika mti mbichi, mkawa nanyi kwa (mti) huo mnauwasha.

81. Je, yule aliyeziumba mbingu na ardhi (mnaona) hana uweza wa kuumba (mara ya pili) mfano wao (wanadamu)? Kwa nini? Naye ni Mwumbaji mkuu, Mjuzi (wa kila jambo).

82. Hakika amri yake anapotaka cho chote (kile kitokee) ni kukiambia: ‘Kuwa,’ basi mara huwa.

83. Ametukuka yule ambaye mkononi mwake umo ufalme wa kila kitu; na kwake mtarejezwa nyote.

وَاتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ آلِهَةً لَعَلَّهُمْ يَنْصَرُونَ ﴿٧٤﴾

لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَهُمْ وَهُمْ لَهُمْ جُنْدٌ مُحَضَّرُونَ ﴿٧٥﴾

فَلَا يَخْرُجُكَ قَوْلُهُمْ مَرَاتًا نَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٧٦﴾

أَوَلَمْ يَرَ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُبِينٌ ﴿٧٧﴾

وَضَرَبَ كِتَابًا مَثَلًا لِنَبِيِّ خَلَقْنَاهُ قَالَ مَنْ نَبِيِّ الْعِظَامِ وَهِيَ رَعِيمٌ ﴿٧٨﴾


قُلْ يُجِيبُهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾

الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ مِنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنْتُمْ مِنْهُ تُوقَدُونَ ﴿٨٠﴾

أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ ﴿٨١﴾

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾

فَسُبْحَانَ الَّذِي بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾



Ina Aya 182

**SURATUS SAAFFAT**  
(Imeteremka Makka)

Ina Makara 5

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa (wale Malaika) wajipangao safusafu

وَالصَّفَاتِ صَفًا

2. Tena kwa wale wanaokataza mabaya

قَالَتْ جِرَتْ زَجْرًا

3. Kisha kwa wale wasomao mawaidha (ya Mwenyezi Mungu)

فَالشَّيْبِ ذِكْرًا

4. Kwa yakini Mungu wenu ni Mmoja tu.

إِنَّ إِلَهَكُمْ لَوَاحِدٌ

5. Mola wa mbingu na ardhi na yaliyomo kati yake, (yao); na ni Mola wa mashariki zote (na magharibi zake).

رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَرَبُّ الْمَشَارِقِ

6. Bila shaka sisi tumeipamba mbingu ya karibu (hii) kwa pambo la nyota

إِنَّا رَبَّنَا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِرِيَّةٍ الْكَوَاكِبِ

7. Na kuilinda na kila shetani asi.

وَحَقَّقْنَا مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ مَّارِدًا

2-4. Wamepachika yasiyokusudiwa katika maelezo ya Aya walizozitia nambari huzi.

5. Mwenyezi Mungu katika Aya nyingine — kama Aya ya 9 ya *Suratul Muzzammil* — amejita *Rabbul Mashriq wal Maghribi*. Na katika Aya nyingine — kama Aya ya 17 ya *Suratur Rahman* — amejita *Raabul Mashriqayni wa Rabbul Maghribayn*. Na katika Aya nyingine — kama Aya ya 40 ya *Suratul Maarij* — amejita *Rabbul Mashaariqi wal Maghaaribi*. Ile ya kwanza *Rabbul Mashriqi wal Maghribi* yaani Mola wa Kunakotokea jua na kunakochwea jua. Na ile ya pili *Rabbul Mashriqayn wa Rabbul Maghribayn* yaani Mola wa kunakotokea jua siku za baridi na siku za joto na Mola wa kunakochwea jua siku za baridi na siku za joto. Isije ikadhaniwa kwa kule kutoka jua upesi siku za joto na kukawia kuchwa na kuchelewa kutoka jua siku za baridi na likachwa upesi kuwa kuna waungu wawili — mmoja anapitisha amri zake siku za joto na mmoja anapitisha amri zake siku za baridi. Basi Mwenyezi Mungu ni huyo huyo mmoja tu; lakini — kwa maslaha ya viumbe vyake — mara anawafanyia hivi, na mara anawafanyia vile. Na vile kusema hapa *Rabbul Mashaariqi wal Maghaaribi* yaani Mola wa Matokeo ya jua mbali mbali na machweo ya jua mbali mbali ulimwengu mzima, ndiyo kama hivi tunavyojua sasa kwa haya maredio kuwa likiwa linachomoza jua kwetu sasa hivi, kwengine limekwisha chomoza, ima zamani au karibu hivi au karibu sana au bado. Na linapokuchwa ndiyo vile vile. Na linapopinduka upande wa pili ni vile vile. Basi Mwenyezi Mungu anasema kuwa Mola wa kote huko ni huyo huyo tu Mwenyezi Mungu peke yake — *Wahdahuu Laa Sharyka Lahuu*. Na haya ya kujua kuwa jua linakuchwa na kuchomoza nyakati mbali mbali ndiyo kwanza yajulikane sasa; na Qurani imetaja habari hii zaidi ya myaka alfu sasa. Ukweli wa Qurani unazidi kudhihiri tu. Utango nautambae.

7. Wamegeuza tena muradi wa Mwenyezi Mungu katika tamko la Shetani kama walivyogeuza muradi wa tamko la Jini, wakasema kuwa muradi wa maneno yote mawili haya ni binadamu wabaya, sio viumbe wengine. Tumeyabainisha haya katika Aya ya 112 ya *Suratul An-Am* na katika pengine pengi kabisa. Na wamegeuza muradi wa Aya zote hizi walizozifanya 8-11.

8. Wasiweze kusikiliza (yanayosemwa na hao) viumbe watukufu (Malaika); na wanafukuzwa huko kila upande.

9. Kwa hizaya; na wanayo adhabu (inayowazuia kufika huko) inayodumu kwao

10. Isipokuwa anayenyakuwa kitu kidogo hivi (katika maneno yanayosemwa huko); mara kikamfuata kimondo (kijinga cha moto) king'aracho (kikamuangamizilia mbali).

11. Hebu waulize, "Je, wao (binadamu) ni wenye umbo gumu zaidi au wale (wengine) tuliowaumba (kama tulivyokuumbeni nyinyi, kama Malaika na Majini . . .)?" Bila shaka sisi tuliwaumba (wanaadamu) kwa udongo unaonata. (Wana nguvu gani za kujivunia)?

12. Bali unastaajabu, na wao wanafanya mzaha.

13. Na wanapoonywa hawaonyeki.

14. Na wanapoiona miujiza hufanya mzaha.

15. Na wanasema "Hayakuwa haya (anayotuonyesha Muhammad) ila ni uchawi ulio dhahiri."

16. "Oh! tutakapokufa na kuwa udongo na mifupa ndiyo kweli tutafufuliwa?"

17. "Hata wazee wetu wa zamani (pia watafufuliwa? Uwongo huo)."

18. Sema: "Naam (mtafufuliwa), na hali ya kuwa mumo katika hizaya."

19. Huko (kufufuliwa) kutakuwa ni Ukelele mmoja tu, mara wanaona (Kiama kimefika).

20. Wasema: "Ole wetu! Hii ndiyo (ile) siku ya Malipo!"

21. (Waambiwe:) "Hii ndiyo siku ya Hukumu mliyokuwa mkiikadhibisha."

22. (Kusemwe:) "Wakusanyeni wale waliodhulumu (nafsi zao) pamoja na wenzi wao na wale waliokuwa wakiwaabudu "

23. "Badala ya Mwenyezi Mungu; Waongozeni njia ya Jahanamu."

24. "Na wasimamisheni (hapo); hakika wataulizwa "

25. (Waambiwe:) "Muna nini? Mbona hamnusuriani?"

لَا يَسْمَعُونَ إِلَى الْمَلَأِ الْأَعْلَى وَيُقَدِّفُونَ مِنْ كُلِّ  
جَانِبٍ ﴿٣٨﴾

دُحُورًا وَلَهُمْ عَذَابٌ وَأَصِيبٌ ﴿٣٩﴾

إِلَّا مَنْ خِطَفَ الْحَظْفَةَ فَاتَّبَعَهُ شَهَابٌ ثَائِبٌ ﴿٤٠﴾

فَأَسْتَفْتِيهِمْ أَهْمُ أَشَدُّ خَلْقًا أَمْ مَنْ خَلَقْنَا، إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ  
مِّنْ طِينٍ لَّازِبٍ ﴿٤١﴾

بَلْ عَجِبْتَ وَيَسْخَرُونَ ﴿٤٢﴾

وَإِذَا ذُكِّرُوا لَا يَذَكَّرُونَ ﴿٤٣﴾

وَإِذَا رَأَوْا آيَةً يَسْتَسْخِرُونَ ﴿٤٤﴾

وَقَالُوا إِن هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٤٥﴾

وَإِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظَامًا، إِنَّا لَبَصُورُونَ ﴿٤٦﴾

أَوَابًا وَإِنَّا لَأَوَّلُونَ ﴿٤٧﴾

قُلْ نَعَمْ وَأَنْتُمْ دَاخِرُونَ ﴿٤٨﴾

فَأَمَّا هِيَ فَرْجَةٌ وَاحِدَةٌ فَأِذَا هُمْ يَنْظُرُونَ ﴿٤٩﴾

وَقَالُوا يَا وَيْلَنَا هَذَا يَوْمُ الدِّينِ ﴿٥٠﴾

﴿٥١﴾ هَذَا يَوْمُ الْفَصْلِ الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٥٢﴾

أَحْشَرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ وَمَا كَانُوا

يَعْبُدُونَ ﴿٥٣﴾

﴿٥٤﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَأَهْدُوهُمْ إِلَى صِرَاطِ الْجَحِيمِ ﴿٥٥﴾

وَقِفُّهُمْ إِنَّهُمْ مَسْئُولُونَ ﴿٥٦﴾

مَا كُنْتُمْ لَكُمْ تَنَاصُرُونَ ﴿٥٧﴾

26. Siku hiyo watadhalilika kabisa.
27. Wataingia kuulizana wao kwa wao.
28. Waseme: (kuwaambia wale wakubwa wao) "Kwa hakika nyinyi mlikuwa mkitujia kwa njia za kheri, (kumbe mkitutakia shari)!"
29. Waseme (wale wakubwa): "Bali nyinyi wenyewe hamkuwa Waislamu."
30. "Hatukuwa na mamlaka juu yenu (ya kukutoeni katika Uislamu); bali nyinyi wenyewe mlikuwa wapotofu (wapotevu)."
31. "Basi hukumu ya Mola wetu imekwisha tuthubutikia, bila shaka tutaonja (tu adhabu ya Mwenyezi Mungu)."
32. "Tulikupotezeni (kwa sababu) sisi wenyewe tulikuwa wapotofu (wapotevu)."
33. Basi wao kwa hakika siku hiyo watakuwa katika adhabu pamoja.
34. Hivyo ndivyo tutakavyowafanya maasi.
35. Wao, walipokuwa wakiambiwa, "Hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu," walikuwa wakikataa
36. Na husema: "Oh! Tuiache miungu yetu kwa ajili ya (huyu) mtunga mashairi mwendawazimu?"
37. (Nabii Muhammad si mtunga mashairi, mwendawazimu) bali ameleta haki na amewasadikisha Mitume (waliotangulia).
38. Hakika nyinyi bila shaka mtaionja adhabu iumizayo.
39. Wala hamtalipwa ila yale mliyokuwa mkiyafanya
40. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliotengenezwa (waliotengeneza amali zao).
41. Hao ndio watakaopata riziki maalumu
42. Matunda (ya kila namna), na watahishimiwa
43. Katika mabustani za neema
44. Wako juu ya vitanda (viti vya enzi vya fahari), wamekabiliana (wanazungumza).
45. Wanazungushiwa gilasi zenye (vinywaji) safi

بَلْ هُمْ الْيَوْمَ مُتَسَلِّمُونَ ﴿٢٦﴾  
 وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٢٧﴾  
 قَالُوا إِنَّكُم كُنْتُمْ تَأْتُونَنَا عِنَ الْيَمِينِ ﴿٢٨﴾

قَالُوا بَلْ لَمْ نَكُونُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٢٩﴾

وَمَا كَانَ لَنَا عَلَيْكُم مِّنْ سُلْطٰنٍ بَلْ كُنْتُمْ قَوْمًا طٰغِينَ ﴿٣٠﴾

فَحَقَّ عَلَيْنَا قَوْلُ رَبِّنَا إِنَّا لَذٰلِقُونَ ﴿٣١﴾

فَأَعْوَبْنٰكُمْ إِنَّا كُنَّا غٰوِبِينَ ﴿٣٢﴾

فَأَنهٖم يَوْمَئِذٍ فِي الْعَذَابِ مُشْتَرِكُونَ ﴿٣٣﴾

إِنَّا كَذٰلِكَ نَفْعَلُ بِالْجٰرِمِينَ ﴿٣٤﴾  
 إِنهٖم كٰنُوْا إِذًا قٰوِيْلٌ لَّهٖم لَّا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٣٥﴾

وَيَقُولُوْنَ إِنَّا لَنَرٰكُم كَوٰلِهِنَا بِشَاعِرٍ مَّجْنُوْنٍ ﴿٣٦﴾

بَلْ جَآءَ بِالْحَقِّ وَصَدَقَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٧﴾

إِنكُم لَذٰلِقُوْا الْعَذَابِ الْاَلِيمِ ﴿٣٨﴾

وَمَا تُجْرَوْنَ اِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣٩﴾

اِلَّا عِبَادَ اللّٰهِ الْخٰلِصِيْنَ ﴿٤٠﴾

اُولٰٓئِكَ لَهُمْ رِزْقٌ مَّعْلُوْمٌ ﴿٤١﴾

فَوَاكِهٍ وَهٖم مُّكْدَمُوْنَ ﴿٤٢﴾

فِيْ جَنَّٰتٍ النَّعِيْمِ ﴿٤٣﴾

عَلٰى سُرُرٍ مُّتَقٰبِلِيْنَ ﴿٤٤﴾

يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِكَأْسٍ مِّنْ مَّعِيْنٍ ﴿٤٥﴾

46. Vyeupe vyenye ladha kwa hao wavinywao;

بَيْضَاءَ لَدَى الشَّرِيبِ ۝

47. Kwa vinywaji hivyo hautakuwa udhia wala kuondokwa na akili.

لَا فِيهَا غَوْلٌ وَلَا هُمْ عَنْهَا يُنْزَفُونَ ۝

48. Na pamoja nao watakuwa wanawake wenye macho mazuri makubwa

وَعِنْدَهُمْ قَصْرٌ الطَّرْفِ عَيْنٍ ۝

49. (Safi) wanawake hao kama mayai (ya mbuni) yaliyohifadhiwa.

كَأَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَّكْنُونٌ ۝

50. Waingie kuulizana wenyewe kwa wenyewe.

فَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ۝

51. Aseme msemaji mmoja miongoni mwao: "Hakika nilikuwa na rafiki"

قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ إِنِّي كَانَ لِي قَرِينٌ ۝

52. Aliyekuwa akinambia:— "Ah! Wewe ni katika wale wanaosadiki."

يَقُولُ أَهْلِكَ لِمَنِ الْمُصَدِّقِينَ ۝

53. "Ya kuwa tutakapokufa na tukawa udongo na mifupa (tutafufuliwa) tulipwe (kwa tuliyoyafanya kama anavyosema Muhammad)?"

إِذَا دُئِنَّا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظَامًا عَرَانَا كَمَدَّيْنُونَ ۝

54. Atasema: "Je, Mtamchungulia (huko Motoni, tumuone namna anavyoadhibiwa)?"

قَالَ هَلْ أَنْتُمْ مُطَّلِعُونَ ۝

55. Basi atachungulia na atamuona katikati ya Jahanamu.

فَأَطْلَمَ فَرَأَاهُ فِي سَوَاءٍ أَبْحِيمٍ ۝

56. Amwambie: "Wallahi! Ulikurubia kunipoteza"

قَالَ سَاءَ اللَّهُ إِنَّ كَيْدَكَ لَشَدِيدٌ ۝

57. "Na lau si neema ya Mola wangu, bila shaka ningalikuwa miongoni mwa waliohudhurishwa (humo Motoni kama wewe)."

وَلَوْلَا نِعْمَةُ رَبِّي لَكُنْتُ مِنَ الْمُحْضَرِينَ ۝

58. "Je, sisi ni wenye kufa tena?"

أَفَمَا نَحْنُ بِمَبْتَلِينَ ۝

59. "Ila kifo chetu cha kwanza! (Kinyume chenu nyinyi) Wala sisi hatutaadhibiwa."

إِلَّا مَوْتَنَا الْأُولَىٰ وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِينَ ۝

60. Bila shaka huku ndiko kufuzu (kufaulu), kukubwa.

إِنَّ هَذَا هُوَ الْقَوْمُ الْعَظِيمُ ۝

61. Basi mfano wa haya ndiyo wafanye hao wafanyao.

لِيُثَلَّ هَذَا فَلَئِمِلَ الْعِمْلُونَ ۝

62. Je, karibisho la namna hii silo bora au kupata mti wa zakkum? (Mti mchungu kabisa watakaolishwa watu wa Motoni).

أَذَلِكَ خَيْرٌ نُزُلًا أَمْ شَجَرَةُ الزَّكَاةِ ۝

62. Kwa ajili ya kukataa kwao mambo anayoyataja Mwenyezi Mungu yasiyolingia katika akili zao ndogo na ilimu zao chache — wameupinga huo *Mshajaratuz Zaqqum*, na wameupinga mahala pengine kama Aya ya 43 ya *Suratul Dhukhaan* na Aya ya 52 ya *Suratul Waaqiah*. Wakasema kuwa tamko hili ni ufupisho wa Aya *Dhuq Innaka Antal Azyzul Karym*. Tazama unafiki huu. Hakuna mtu yoyote kabla yao aliyezua uwongo huu. Nawatazame tafsiri zote za ulimwengu mzima.

63. Kwa Yakini sisi tumeufanya ni adhabu ya (hao) madhalimu (wa nafsi zao).

إِنَّا جَعَلْنَاهَا فِتْنَةً لِلظَّالِمِينَ ﴿٣٧﴾

64. Hakika huo ni mti unaotoka (unaoota) katikati ya Jahanamu

إِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ ﴿٣٨﴾

65. (Panda za) Matunda yake (zinatisha) kama kwamba ni vichwa vya mashetani.

طَلَعَهَا كَأَنَّه رُؤُوسُ الشَّيْطَانِ ﴿٣٩﴾

66. Bila shaka wao watakula katika (mti) huo, na kwa huo wajaze matumbo (yao).

فَأَنَّهُمْ لَأَكَلُونَ مِنْهَا وَمِنْهَا الْبُطُونَ ﴿٤٠﴾

67. Kisha bila shaka utawathubutikia, juu ya uchungu wa mti huo, mchanganyiko wa maji ya moto.

ثُمَّ إِنَّ لَهُمْ عَلَيْهَا لَشَوْبًا مِّنْ حَمِيمٍ ﴿٤١﴾

68. Halafu, kwa yakini, marejeo yao yatakuwa (huko huko) katika Jahanamu, (hawana mahala pengine).

ثُمَّ إِنَّ مَرْجِعَهُمْ لَإِلَى الْجَحِيمِ ﴿٤٢﴾

69. Hakika wao waliwakuta baba zao wamepotea.

إِنَّهُمْ أَلفُوا آبَاءَهُمْ ضَالِّينَ ﴿٤٣﴾

70. Na wao pia wakaendeshwa kufuata nyayo zao, (wakakataa kusikiliza maneno ya Mtume).

فَهُمْ عَلَىٰ أَثَرِهِمْ يُهْرَعُونَ ﴿٤٤﴾

71. Na bila shaka watu wengi wa zamani walipotea kabla yao.

وَلَقَدْ صَلَّ قَبْلَهُمْ أَكْثَرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٤٥﴾

72. Na hakika tulipeleka waonyaji kwa watu hao; (lakini walikataa kutii).

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا فِيهِمْ مُّنذِرِينَ ﴿٤٦﴾

73. Basi tazama ulikuwaje mwisho wa wale walioonywa (wasionyeke)?

فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُنذَرِينَ ﴿٤٧﴾

74. Isipokuwa watumwa wa Mwenyezi Mungu waliotengenezwa, (waliotengeneza amali zao); (hao ni watu wa Peponi tu).

إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿٤٨﴾

75. Na kwa yakini Nuhu alitwita (tumnusuru); (tukamwitikia kwa vizuri kabisa). Basi ni waitikiaji wema tulioje sisi!

وَلَقَدْ نَادَيْنَا نُوْحًا فَلَنِعْمَ الْمُجِيبُونَ ﴿٤٩﴾

76. Na tulimuokoa yeye na watu wake katika msiba mkubwa (wa tufani lililoharikisha kila kitu).

وَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ ﴿٥٠﴾

77. Na tuliwajaalia kizazi chake wawe ndio wenyewe kubaki (mpaka leo ulimwenguni).

وَجَعَلْنَا ذُرِّيَّتَهُ هُمُ الْبَاقِينَ ﴿٥١﴾

65. Qurani imeteremshwa kwa lugha ya Kiarabu. Basi kwa hivyo inatumia katika lugha yake matumizi ya Kiarabu. Na wao walikuwa wanashabihisha kibaya kwa sura ya Shetani.

78. Na tukamuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) waliokuja baadaye.

79. Amani kwa Nuhu ulimwenguni kote.

80. Kwa hakika hivi ndivyo tuwalipavyo wafanyao wema.

81. Kwa hakika yeye alikuwa katika waja wetu walioamini (vizuri kabisa).

82. Kisha tukawagharikisha wale wengine.

83. Na hakika Ibrahimu alikuwa katika kundi lake, (akenda mwendo wake).

84. Aliiendea (dini ya) Mola wake kwa moyo safi.

85. Alimwambia baba yake na watu wake, "Mnaabudu nini?"

86. "Oh! Kwa uzushi tu, miungu badala ya Mwenyezi Mungu — ndiyo mnayoitaka?"

87. "Basi nini fikira yenu juu ya Mola wa walimwengu wote? (Mnamuona hatoshelezi ndio mnatafuta waungu wengine?)"

88. Kisha akatazama mtazamo (mkubwa) katika nyota (akasema "Nitachukua fursa ya kuwajulisha uwongo wa dini yao kwa kuwaonyesha kuchomoza kwake hizo nyota wanazoziaabudu na kuchwa kwake)."

89. Akasema: "Hakika mimi ni mgonjwa."

90. Nao wakamuacha, wakampa kisogo (wakenda zao viungani katika mandari zao).

91. Basi alikwenda kwa siri kwa miungu yao akaiambia (kwa stihzai): "Muna nini? Mbona hamuli? (Vyakula hivi vya mihanga mlivyowekewa?)"

92. "Mumekuwaje! Hamsemi?"

93. Kisha akawageukia kuwapiga kwa mkono wa kulia, (kwa mwisho wa nguvu zake).

94. (Basi waliposikia wenyewe) wakamjia upesi upesi (wakamwambia kwa nini kuwavunja waungu wao).

95. Akasema: "Oh! Mnaviabudu mnavyovichonga (wenyewe kwa mikono yenu)?"

96. "Hali Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuumbeni nyinyi na mnavyovifanya."

وَتَرْكُنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿٧٨﴾

سَلِّمْ عَلَى نُوحٍ فِي الْعَالَمِينَ ﴿٧٩﴾

إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٠﴾

إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨١﴾

ثُمَّ أَعْرَفْنَا الْآخِرِينَ ﴿٨٢﴾

وَأَنَّ مِنْ شِيعَتِهِ لَإِبْرَاهِيمَ ﴿٨٣﴾

إِذْ جَاءَ رَبَّهُ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ ﴿٨٤﴾

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَاذَا تَعْبُدُونَ ﴿٨٥﴾

أَفَبِمَا آتَى الْهَيْهَاتَهُ دُونَ اللَّهِ تُرِيدُونَ ﴿٨٦﴾

فَمَا تَطَّلَعُكُمْ بِهِ الْعَالَمِينَ ﴿٨٧﴾

فَنظَرَ نَظْرَةً فِي النُّجُومِ ﴿٨٨﴾

فَقَالَ إِنِّي سَقِيمٌ ﴿٨٩﴾

فَتَوَلَّوْا عَنْهُ مُدْبِرِينَ ﴿٩٠﴾

فَرَاغَ إِلَىٰ آلِهِمُ فَقَالَ آتَاكُمْ لُونَ ﴿٩١﴾

مَا لَكُمْ لَا تَنْطِقُونَ ﴿٩٢﴾

فَرَأَىٰ عَلَيْهِمْ صُرُبًا بِالْيَمِينِ ﴿٩٣﴾

فَأَقْبَلُوا إِلَيْهِ يَزْفُونَ ﴿٩٤﴾

قَالَ أَعْبُدُونَ مَا تَحْتُمُونَ ﴿٩٥﴾

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾

97. Wakasema: "Mjengeeni jengo (mlitie makuni mliwashe moto), kisha mtupeni motoni humo."

98. Basi walitaka kumfanyia vitimbi (vya kumua), lakini tukawafanya wao kuwa wadhhalifu. (Moto ule haukumuunguza hata chembe Nabii Ibrahimu.)

99. Na (Ibrahimu) akasema: "(Naondoka nchi hii). Nakwenda (Shamu nchi aliyoniamrisha) Mola wangu. Ndiye atakayeniongoza (na kunitengezea kila yangu)."

100. "Ee Mola wangu! Nipe (mtoto awe) miongoni mwa watenda mema."

101. Ndipo tukampa habari njema ya (kuwa atapata) mtoto mpole. (Basi akapata. Naye ndiye Nabii Ismaili).

102. Basi alipofikia (makamu ya) kwenda na kurudi pamoja naye, alimwambia: "Ee mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. (Na ndoto ya Mitume ni Wahyi). Basi fikiri, waonaje?" Akasema: "Ee baba yangu! Fanya unayoamrisha, utanikuta Inshallah miongoni mwa wanaosubiri."

103. Basi wote wawili walipojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu), na akamlaza kifudufudi (amchinje).

104. Pale pale tulimwita: "Ewe Ibrahimu:"

105. "Umekwishasadikisha ndoto. (Usimchinje mwanao)." Kwa yakini hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema.

106. Bila shaka (Jambo) hii ni jaribio lililo dhahiri, (mihani ulio dhahiri).

107. Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu.

قَالُوا ابْنُوا لَهُ بُيُوتًا فَأَلْقُوهُ فِي الْجَحِيمِ ۝

فَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَسْفَلِينَ ۝

وَقَالَ إِنِّي ذَاهِبٌ إِلَىٰ رَبِّي سَيَهْدِينِ ۝

رَبِّ هَبْ لِي مِن الطَّالِحِينَ ۝

فَبَشَّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ ۝

فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعْيَ قَالَ يَبْنَؤُا إِنِّي أُرَىٰ  
فِي الْمَنَامِ أَنِّي أَذْبَحُكَ فَانظُرْ مَاذَا تَرَىٰ ۚ قَالَ  
يَأْتِيكَ أَفْعَلٌ مَا تُؤْمَرُ سَتَجِدُنِي إِن شَاءَ اللَّهُ مِنَ  
الطَّائِرِينَ ۝

فَلَمَّا أَسْلَمَا وَتَلَّهُ لِلْجَبِينِ ۝

وَنَادَيْنَاهُ أَنِ يَا إِبْرَاهِيمُ ۝

قَدْ صَدَّقْتَ الرُّؤْيَا إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي  
الْمُحْسِنِينَ ۝

إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْبَلَاءُ الْمُبِينُ ۝

وَقَدَيْنَاهُ بِذِي عَظِيمٍ ۝

102. Hapa tunaonyesha mithali bora ya mja kumtii Mola wake, na ya mtoto kumtii mzee wake. Nabii Ibrahimu anaamrisha kumchinja mtoto wake kwa mkono wake, naye akawa tayari kufuata amri. Na mtoto akakubali kuchinjwa.

103-107. Yaani walipokuwa tayari wote wawili kufuata amri ya Mola wao, na Nabii Ibrahimu akamlaza mwanawe ili amchinje. Mwenyezi Mungu alimsamehe na akamkomboa mtoto huyo kwa mnyama. Na hapo ndipo ilipochukuliwa Sunna ya kuchinja mnyama katika Idil-Haj kwa Wa-Islamu wote na ikadumu mpaka leo.

Mtume Muhammad s.a.w. ni katika kizazi cha huyu Nabii Ismaili ambaye alitaka kuchinjwa kisha akaokolewa. Na vile vile baba yake Mtume s.a.w. (Bw. Abdulla) alitaka kuchinjwa, kisha akaokolewa. Kwa hivyo mtume s.a.w. huitwa "Ibnudh Dhabyhayn;" yaani mtoto wa wachinjwa wawili.

108. Na tukamuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) waliokuja baadaye.

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ۝

109. Amani kwa Ibrahimu.

سَلَامٌ عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ۝

110. Hivi ndivyo tunawalipa watendao mema.

كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ۝

111. Bila shaka yeye alikuwa miongoni mwa waja wetu walioamini (kweli kweli).

إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ۝

112. Tena tukambashiria (kumzaa) Is-haka, (mtoto wake wa pili). Nabii miongoni mwa watu wema (kabisa).

وَبَشِّرْنَاهُ بِإِسْحَاقَ نَبِيًّا مِنَ الصَّالِحِينَ ۝

113. Na tukambarikia yeye na Is-haka. Na katika kizazi chao walitokea watendao mema na wanaodhulumu nafsi zao waziwazi. (Kizaliwa na watu wema si hoja hiyo — Sharti na yeye mwenyewe awe mwema ndipo atakapopata wema).

وَبَارَكْنَا عَلَيْهِ وَعَلَىٰ إِسْحَاقَ ۚ وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِمَا مُحْسِنٌ وَعِظِيمٌ ۝

114. Na kwa hakika tuliwafanyia ihsani Musa na Haruni.

وَلَقَدْ مَنَنَّا عَلَىٰ مُوسَىٰ وَهَارُونَ ۝

115. Na tukawaokoa wao na watu wao katika taabu kubwa.

وَنَجَّيْنَاهُمَا وَقَوْمَهُمَا مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ ۝

116. Na tukawanusuru. Basi wakawa wenye kushinda.

وَنَصَّرْنَاهُمْ فَمَا نَأْوَاهُمُ الْعِلْدِينَ ۝

117. Nao wote wawili tukawapa Kitabu kibainishacho (kila linalohitajiwa).

وَآتَيْنَاهُمَا الْكِتَابَ الْمُسْتَبِينَ ۝

118. Na tukawaongoza katika njia iliyonyooka.

وَهَدَيْنَاهُمَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ۝

119. Kisha tukawaachia (sifa nzuri) katika (watu wote) waliokuja baadaye

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِمَا فِي الْآخِرِينَ ۝

120. Amani kwa Musa na Haruni.

سَلَامٌ عَلَىٰ مُوسَىٰ وَهَارُونَ ۝

121. Bila shaka hivi ndivyo tunavyowalipa wafanyao mema.

إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ۝

122. Kwa yakini wao walikuwa miongoni mwa waja wetu walioamini (kweli kweli).

إِنَّهُمَا مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ۝

123. Na hakika Ilyasi alikuwa miongoni mwa Mitume.

وَإِنَّ إِلْيَاسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ۝

124. (Wakumbushe watu) Alipowaambia watu wake: "Oh! hamuogopi?"

إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَلَا تَتَّقُونَ ۝

123. Katika Aya 130 ya Sura hii hii Nabii Ilyasi ameitwa "Ilyasin". Na ndiye huyo huyo Ilyasi. Katika hii Aya waliyoifanya ya 124 wamejidai kutaja itikadi ya Mayahudi ili tuwache itikadi yetu aliyotwambia Mtume ya kurejea Nabii Isa mwisho wa ulimwengu.

125. "Mnamuomba (na kumuabudu) Bali na mnamuacha aliye Mbora wa waumbaji (na ndiye Muumbaji peke yake)."

126. "Mwenyezi Mungu — Mola wenu na Mola wa wazee wenu wa mwanzo!"

127. Wakamkadhibisha: Basi bila shaka watahudhurishwa (adhabuni)

128. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliosafishwa (na Mwenyezi Mungu).

129. Na tumemuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) waliokuja baadaye.

130. Amani kwa Ilyasi.

131. Bila shaka hivi ndivyo tunavyowalipa wafanyao wema.

132. Kwa yakini yeye alikuwa miongoni mwa waja wetu walioamini (kweli kweli).

133. Na kwa hakika Luti alikuwa miongoni mwa Mitume.

134. (Kumbukeni) tulipomuokoa yeye na watu wake wote

135. Isipokuwa mwanamke mkongwe katika wale waliobaki nyuma. (Naye ni mkewe. Bibi huyu hakuwa Muislamu).

136. Kisha tukawaangamiza (wale) wengine (waliokuwa wabaya).

137. Na kwa yakini mnawapita (mnaipitia nchi yao) asubuhi

138. Na usiku (pia). Basi je! Hamfahamu?

139. Na hakika Yunusi alikuwa miongoni mwa Mitume.

140. (Kumbukeni) alipokimbilia katika jahazi iliyosheheni

اتَّبَعُونَ بَعْلًا وَتَذَرُونَ أَحْسَنَ الْخَالِقِينَ ﴿١٢٥﴾

اللَّهُ رَبُّكُمْ وَ رَبُّ آبَائِكُمُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٢٦﴾

فَكَذَّبُوهُ فَأَنَّهُمْ كَمُحَضَّرُونَ ﴿١٢٧﴾

إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلَصِينَ ﴿١٢٨﴾

وَوَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿١٢٩﴾

سَلَامٌ عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿١٣٠﴾

إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣١﴾

إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٣٢﴾

وَإِنَّ لُوطًا لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٣٣﴾

إِذْ جَاءَتْهُ وَأَهْلَهُ أَجْمَعِينَ ﴿١٣٤﴾

إِلَّا نَجْوَىٰ فِي الْغَيْبِينَ ﴿١٣٥﴾

ثُمَّ دَكَّمْنَاهُ الْآخِرِينَ ﴿١٣٦﴾

وَإِنَّكُمْ لَتَمُرُّونَ عَلَيْهِمْ مُصْبِحِينَ ﴿١٣٧﴾

وَبِاللَّيْلِ إِذَا فَلَ تَتَقَلَّبُونَ ﴿١٣٨﴾

وَإِنَّ يُونُسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٣٩﴾

إِذْ أَبَقَ إِلَى الْفَالِكِ الْمَشْحُونِ ﴿١٤٠﴾

140. Mtume Yunusi alipelekwa Ninawah. Watu wa hapo wasiamini. Mwenyezi Mungu akampa amri kuwapa habari kwamba ndani ya muda maalumu itawashukia adhabu. Muda ulipokaribia Nabii Yunusi akatoka nje ya mji ili ikishuka adhabu, yeye isimpate. Wakati ulipofika, watu wale wakaona adhabu inawajia. Hapo wakayakinisha kwamba Yunusi alikuwa Mtume wa haki; wakaamini na kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, naye kwa rehema yake akaiondoshwa adhabu hiyo. Nabii Yunusi hakujua yaliyopita nyuma yake. Alipoona adhabu haikushuka alichelea kuwa watu hao watazidi kumkanusha. Akakimbilia pwani ambako alipata jahazi akaingia. Waliomo katika marikebu hiyo wakawa wamezidi, na chombo kisiweze kwenda. Ikapigwa kura ili itakae muangukia atoswe baharini. Ikamuangukia Nabii Yunusi akatoswa baharini, akamezwa na samaki.

141. Na wakapiga kura. (Na akaingia naye katika kura). Basi akawa miongoni mwa walioshindwa (ikapasa atupwe baharini).

فَأَهِمَّ فَكَانَ مِنَ الْمُدْحَضِينَ ﴿١٤١﴾

142. Mara samaki alimmeza hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa.

فَأَلْتَمَمَهُ الْحَوْتُ وَهُوَ مُلِيمٌ ﴿١٤٢﴾

143. Basi isingelikuwa ya kwamba yeye alikuwa ni miongoni mwa waliokuwa wanamuabudu (Mwenyezi Mungu vilivyo)

فَلَوْلَا أَنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِينَ ﴿١٤٣﴾

144. Bila shaka angalika tumboni mwake mpaka siku watakayofufuliwa (viumbe).

لَكَيْتَ فِي بَطْنِهِ إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٤٤﴾

145. Lakini tukamtupa ufukoni (ufuoni) (kumtoa matumboni mwa huyo samaki), hali ya kuwa mgonjwa.

فَبَدَدْنَا بِالْعَرَاءِ وَهُوَ سَقِيمٌ ﴿١٤٥﴾

146. Na tukamuoteshea mmea wa mbatikhi (akawa anakula).

وَأَنْبَتْنَا عَلَيْهِ شَجَرَةً مِّنْ يَقْطِينٍ ﴿١٤٦﴾

147. Na tulimpeleka kwa (watu) laki moja au zaidi, (wale wale watu wake).

وَ أَرْسَلْنَاهُ إِلَى مِائَةِ آلَافٍ أَوْ يُزِيدُونَ ﴿١٤٧﴾

148. Basi wakaamini na tukawastarchesha mpaka muda (wao wa kufa).

فَأَمَّاؤَا فَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿١٤٨﴾

149. Waulize (Makureshi wanaosema kuwa Mwenyezi Mungu ana watoto wanawake, na hali ya kuwa wao wanawadharau na kuwachukia watoto wanawake. Waambie):- "Oh! Mola wako ndio ana watoto wa kike, na wao wawe wenye watoto wa kiume?"

فَأَسْتَفْتِيهِمُ الرِّبَّكَاتِ الْبَنَاتِ وَكُهُمُ الْبَنُونَ ﴿١٤٩﴾

150. Je! Tumewaumba Malaika kuwa wanawake, nao wakashuhudia? (Ndio maana wanasema kuwa Malaika ni wanawake?).

أَمْ خَلَقْنَا الْمَلَائِكَةَ إِنَاثًا وَهُمْ شَاهِدُونَ ﴿١٥٠﴾

151. Tahadharini Kwa uzushi wao wanasema kuwa:

أَلَا إِنَّهُمْ مِّنْ أَرْكَهَمَ يُقْتُلُونَ ﴿١٥١﴾

152. "Mwenyezi Mungu amezaa." Na hakika wao bila shaka ni waongo.

وَلَدَ اللَّهُ ۗ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿١٥٢﴾

153. Oh! Amechagua watoto wa kike kuliko wa kiume?

أَصْطَفَى الْبَنَاتِ عَلَى الْبَنِينَ ﴿١٥٣﴾

154. Mumekuwaje, Mnahukumu namna gani?

مَا لَكُمْ بِكَيْفِ تَقُولُونَ ﴿١٥٤﴾

155. Oh! Hamkumbuki (kuwa hayana akili haya mnayosema)?

أَفَلَا تَتَذَكَّرُونَ ﴿١٥٥﴾

156. Au muna dalili iliyo wazi (ya haya mnayoyasema?).

أَمْ لَكُمْ سُلْطٰنٌ مُّبِينٌ ﴿١٥٦﴾

157. Basi leteni Kitabu chenu kama mnasema kweli.

فَأَنزَلْنَا بِكِتَابِكُمْ ءِزْرًا كَمَا مَّضَىٰ قَبْلَينَ ﴿١٥٧﴾

158. Na wameweka nasaba baina yake na majini, (wakasema vile vile kuwa Majini ni watoto wa Mwenyezi Mungu). Na majini wamekwishajua hakika wao bila shaka watahudhurishwa (Motoni kwa ubaya wao na kwa kuwa wao ni viumbe wabaya kama viumbe wengine wabaya).

159. Mwenyezi Mungu Yu mbali na sifa wanazompa

160. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliochaguliwa (na Mwenyewe Mwenyezi Mungu; hao ndio wanaojua kumsifu Mwenyezi Mungu).

161. Basi bila shaka nyinyi na mnaowabudu

162. Hamuwezi kuwapoteza

163. Isipokuwa wale watakaolingia Motoni.

164. Na (wanasema Malaika katika kujua cheo chao, kuwa:—) “Hakuna yoyote miongoni mwetu ila anapo mahali pake mahsusi (ma-alumu).”

165. “Na kwa yakini katika sisi wako wajipangao safu (wakasali jamaa).”

166. “Na wako katika sisi wamtukuzao (Mwenyezi Mungu kwa kumkanushia sifa zisizokuwa zake).”

167. Na hakika walikuwa (makafiri wa Kiarabu) wakisema:

168. “Tungalikuwa na kitabu kama walivyo kuwa navyo wale watu wengine wa mwanzo.”

169. “Bila shaka tungalikuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliohalisika (waliosafika).”

170. Lakini (kilipowajia hicho kitabu) walikikanusha. Basi karibuni watajua (nini nitakavyowafanya).

171. Na bila shaka neno letu limekwisha kutangulia kwa waja wetu waliopewa Utume.

172. Ya kuwa wao ndio watakaonusuriwa.

173. Na kuwa jeshi letu ndilo litakaloshinda.

174. Basi waachilie mbali kwa muda mdogo (tu hivi)

175. Na watazame tu; nao sasa hivi wataona.

176. Oh! wanaihimiza adhabu yetu?

وَجَعَلُوا بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْجَنَّةِ نَسَبًا وَلَقَدْ عَلِمَتِ الْجِنَّةُ إِنَّهُمْ لَمُحْضَرُونَ ﴿١٥٨﴾

سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُصِفُونَ ﴿١٥٩﴾

إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلَصِينَ ﴿١٦٠﴾

فَأَنكُم مَّا تَعْبُدُونَ ﴿١٦١﴾

مَّا أَنتُمْ عَلَيْهِ بِفَتَنِينَ ﴿١٦٢﴾

إِلَّا مَن هُوَ صَالِحٌ جَمِيمٌ ﴿١٦٣﴾

وَمَا مِنَّا إِلَّا لَهُ مَقَامٌ مَّعْلُومٌ ﴿١٦٤﴾

وَأِنَّا لَنَحْنُ الصَّافُونَ ﴿١٦٥﴾

وَأِنَّا لَنَحْنُ الْمُسَبِّحُونَ ﴿١٦٦﴾

وَأَن كَانُوا يَقُولُونَ ﴿١٦٧﴾

لَوْ أَنَّا عِنْدَنَا ذِكْرًا مِّنَ الْأَوَّلِينَ ﴿١٦٨﴾

لَكُنَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلَصِينَ ﴿١٦٩﴾

فَكَفَرُوا بِهِ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿١٧٠﴾

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَلِمَتُنَا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿١٧١﴾

إِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنْصُورُونَ ﴿١٧٢﴾

وَإِنَّ جُنْدَنَا لَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿١٧٣﴾

فَقَوْلٌ عَزِيمٌ مِّمَّا جَاءَ حِينَئِذٍ ﴿١٧٤﴾

وَ أُنصِرَهُمْ فَسَوْفَ يُبْصَرُونَ ﴿١٧٥﴾

أَفَعِدْنَا يَا مُتَعَجِّلُونَ ﴿١٧٦﴾

177. Basi (adhabu) itakaposhuka uwanjani kwao (wataangamia tu); itakuwa asubuhi mbaya kwa wale walioonywa (wasionyeye).

178. Na waache tu kwa muda kidogo (tu hivi)

179. Na tazama tu; nao hivi karibuni wataona.

180. Ameepukana Mola wako, Mola Mwenye enzi, na yale wanayomsifu (nayo makafiri).

181. Na amani juu ya Mitume (wa Mwenyezi Mungu).

182. Na sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote.

فَإِذَا نَزَلَ بِسَاطِرِهِمْ فَسَاءَ صَبَابُ الْمُنذَرِينَ ﴿١٧٧﴾


وَتَوَلَّ عَنْهُمْ حَتَّىٰ حَبِيبٍ ﴿١٧٨﴾

وَأَبْصَرَ قَمُوفٌ يُبْصِرُونَ ﴿١٧٩﴾

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿١٨٠﴾

وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ ﴿١٨١﴾

وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٨٢﴾



Ina Aya 88

## SURAT SAD

Ina Makara 5

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuncemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuncemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Sad, Naapa kwa Qurani (hii) yenye mauidha.

ص وَالْقُرْآنِ ذِي الذِّكْرِ ۝

2. Lakini wale waliokufuru wamo katika majivuno na upinzani (ushindani); (hawataki kufuata mauidha hayo).

بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي عَذَابٍ وَشِقَاقٍ ۝

3. Tumeziangamiza uma ngapi kabla yao, wakapiga kelele (wakati huo); lakini wakati wa kuokoka ulikuwa umekwisha kupita.

كَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ قَرْنٍ فَنَادَُوا وَآوَلَاتِ حَيْثَ مَنَّا ۝

4. Na walistaajabu kuwajia Muonyaji anayetokana na wao, wakasema makafiri: "Huyu ni mchawi, muongo."

وَعَجِبُوا أَنْ جَاءَهُمْ مُنذِرٌ مِنْهُمْ وَقَالَ الْكُفْرُونَ هَذَا سِحْرٌ كَذَّابٌ ۝

5. "Oh! Amewafanya miungu (wote) kuwa Mungu mmoja tu! Bila shaka hili ni jambo la ajabu."

أَجْعَلِ اللَّهُ لَهُهُ آيَةً وَإِنِ هَذَا شَيْءٌ عَجَابٌ ۝

6. Na wakaondoka wakubwa wao (wakiwaambia wasikilizaji maneno ya Mtume): "Nendeni (zenu), (msimsikilize huyo) na dumuni na

وَأَنطَلَقَ الْمَلَأُ مِنْهُمْ أَنِ امْشُوا وَاصْبِرُوا عَلَى آلِهَتِكُمْ ۝

4. Katika waliosema yaliyomo katika Aya hii na za baada yake ni Abu Lahabi — ami yake mwenyewe Mtume. Mtume muda wa miaka mitatu tangu kupewa Utume alikuwa analingania watu kwa siri tu — mmoja mmoja — anayemuona kuelekea kusikia. Akawapata wachache aliwapata. Na wachache hao nao wakawa wanaifanya kazi hiyo nao vile vile, kwa siri; na wakawapata wanaowapata.

Baada ya hapo Mtume aliambiwa na Mwenyezi Mungu akhubiri kwa dhahiri. Basi asubuhi moja Mtume aliondoka akapanda juu ya jabali akapiga kelele kuwaita Maqureshi. Maqureshi kusikia ukelele wa Mtume walikimbizana wote huko. Hata Mtume alipoona kuwa wote wamehudhuria hapo aliwaambia:— "Enyi Maqureshi! Mimi niko juu hapa, naona msiyoyaona. Niki kupeni habari kuwa naona jeshi la maadui linakuja kukushambulieni, mtanisadiki, na hali ya kuwa mnajua kuwa mji wetu huu haushambuliwi?" Wakajibu: "Tutakusadiki kwa sababu haimkiniki kwako wewe kusema yasiyokuwa ndiyo. Wewe husemi ila la kweli tu kama tunavyokujua. Kwa hivi kila utakalotwambia ni la kweli tu; haimkiniki kwako kabisa kutwambia lisilokuwa ndilo." Akawaambia: "Basi nakwambieni kuwa dini yenu hii ya masanamu ni batili. Na mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu; nimeletwa nikufundisheni dini ya haki, nikutoeni katika viza vya ukafiri nikuti ni katika nuru ya Uislamu . . ."

Wakaduwa (wakaduala) Maqureshi, wasijue la kusema. Wamejinasisha wenyewe mtegoni, wamenasa. Lakini mtego wa kuwatega kwenda katika haki, katika nafuu yao ya Akhera na dunia. Baada ya kitambo akainuka Ami yake mwenyewe Mtume — Abu Lahabi — ndugu mkubwa wa baba yake akamwambis Mtume: "Umekhasirika Muhammad! Umeyakosa tuliyokuwa tukikufanyia. Tukikuenzi na kukuona-kitu, kumbe wewe si kitu. Ondokelea mbali! Umekwisha kuharibikiwa . . ." Na akawaambia walioko hapo:— "Ondokeleeni mbali! Muacheni mpuuzi huyu . . ." Akayasema na hayo mengine yaliyotajwa hapa na panginepo.

miungu yenu, hakika hili ni jambo (baya) linalotakiwa (kwetu; la kuacha dini yetu tumfuate yeye).

7. "Sisi hatukusikia haya (ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja hata) katika hii mila ya mwisho. Hayakuwa haya (ya kusema Mungu ni mmoja tu) ila uzushi (tu)."

8. "Oh! Yeye tu ameteremshiwa mauidha haya peke yake (ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja tu) pasina sisi kupewa?" Lakini hao wanayo shaka tu juu ya mauidha yangu; bali hawajaionja adhabu yangu (bado; wataona).

9. Je, wanazo wao hazina za rehema za Mola wako Mwenye nguvu, Mpaji, (hata wanakanusha wanasema wewe hukupewa rehema hizo?).

10. Au je, wanao ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao? Basi na wazipande njia za kwenda huko.

11. Hawa (Makureshi juu ya kujidai kwao) ni vijiasikari vitakavyoendeshwa mbio miongoni mwa mapote ya makafiri yaliyoendeshwa mbio zamani.

12. Walikadhibisha kabla yao watu wa Nuhu, na wa Adi na Firauni mwenye (majumba yaliyo kama) vigingi (vya ardhi, Pyramid).

13. Na thamudi na watu wa Luti na watu wa Kichakani (wa Nabii Shuebu). Hayo ndiyo makundi. (Nasi tuliyaangamiza).

14. Hao wote waliwakadhibisha Mitume; basi adhabu yangu ikawathubutikia.

15. Na hawa (Maqureshi) hawangojei ila ukelele mmoja tu usio na taakhira. (Ukipigwa watakufa wote. Na ukija kupigwa tena wafufuke wote).

16. Na husema (kwa stihzai hawa Maqureshi): "Mola wetu! Tuletee sehemu yetu (ya adhabu) kabla ya siku ya Hisabu."

17. Subiri juu ya hayo wanayoyasema, na umkumbuke Mja wetu Daudi mwenye nguvu (katika kuendesha Utume na ufalme); Kwa yakini yeye alikuwa mwelekevu sana.

إِنَّ هَذَا الشَّيْءَ يُبْرَادُ ۝

مَا سَمِعْنَا بِهَذَا فِي الْمَلَأَةِ الْآخِرَةِ ۚ إِنَّ هَذَا إِلَّا خَيْلَانٌ ۝

أَنْزَلَ عَلَيْهِ الذِّكْرَ مِنْ بَيْنِنَا ۚ بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِنْ ذِكْرِنَا ۚ بَلْ لَنَا يَدٌ وَتَوَقَّأَ عَذَابٌ ۝

أَمْ عِنْدَهُمْ خَزَائِنُ رَحْمَةِ رَبِّكَ الْعَزِيزِ الْوَهَّابِ ۝

أَمْ لَهُمْ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَنَا بَيْنَهُمَا فَلْيَرْتَقُوا فِي الْأَسْبَابِ ۝

جُتِدَ مَا هُنَاكَ مَهْرُومٍ مِنَ الْأَحْزَابِ ۝

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَأَعَادُوا فَأَنْزَلْنَا أَزْوَاجَ الْمَائِدِ ۝

وَأَنْزَلْنَا مِنْ قَبْلِهِ لُوطَ وَصَالَةَ ۚ وَجَاءَكَ الْأَحْزَابُ ۝

إِنَّ كُلَّ الْإِلَهِاتِ كُذِّبَتْ فَحَقُّ عِقَابِ ۝

وَمَا يَنْظُرُ هَؤُلَاءِ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً مِمَّا هُمْ قَوَائِدُ ۝

وَقَالُوا رَبَّنَا عَجِّلْ لَنَا نَجَاتَنَا قَبْلَ يَوْمِ الْحِسَابِ ۝

إِصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَادْخُرْ عَبْدَنَا دَاوُدَ ذَا الْأَيْدِ ۝ إِنَّهُ أَوَّابٌ ۝

7. Wanasema kuwa hata Wakristo hawasemi Mwenyezi Mungu mmoja. Basi hawakubali kufuata dini inayopinga dini zote.

18. Hakika sisi tuliitiisha milima (iwe) pamoja naye, ikimtukuza (Mwenyezi Mungu pamoja naye) jioni na asubuhi

إِنَّا سَخَّرْنَا الْجِبَالَ مَعَهُ يُسَبِّحُنَ بِالْعَشِيِّ وَالْإشْرَاقِ ﴿١٨﴾

19. Na pia ndege waliokusanywa (makundi kwa makundi); wote walikuwa wanyenyekevu kwake.

وَالطَّيْرَ مَحْشُورَةً كُلٌّ لَّهُ أَوَّابٌ ﴿١٩﴾

20. Na tukautia nguvu ufalme wake na tukampa ilimu na (akili ya) kukata hukumu

وَشَدَدْنَا مُلْكَهُ وَأَتَيْنَهُ الْحِكْمَةَ وَفَصَّلَ الْخِطَابِ ﴿٢٠﴾

21. Na je imekuwasilia habari ya wagomvi walipopindukia (ukutani kuingia) chumbani (kwake Nabii Daudi)?

وَهَلْ آتَاكَ بُرُؤُا الْعَصَمِ إِذْ تَسَوَّرُوا الْحُرَابَ ﴿٢١﴾

22. Walipomuingilia Daudi na akawaogopa. Wakasema: "Usiogope; (sisi ni) wagombanao wawili, mmoja wetu amemdhulumu mwenziwe; basi tuhukumu, (hukumu baina yetu) kwa haki wala usipendeleo, na utuongoe katika njia iliyo sawa."

إِذْ دَخَلُوا عَلَى دَاوُدَ فَفَزِعَهُ مِنْهُمْ قَالُوا لَا تَخَفْ خَصْمِينَ بَعْضُنَا عَلَى بَعْضٍ فَاحْكُم بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَلَا تُشْطِطْ وَاهْدِنَا إِلَى سَوَاءِ الصِّرَاطِ ﴿٢٢﴾

23. "Hakika huyu ni ndugu yangu; yeye anaokondoo majike tisiini na tisa, na mimi nina kondoo mmoja tu jike (vile vile) lakini amesema, "Nipe huyu wako nikufugie, (na mimi mwenyewe sitaki), na amenishinda katika maneno."

إِنَّ هَذَا أَخِي لَهُ تِسْعٌ وَتِسْعُونَ نَجَةً وَوَلِي نَجَةٌ وَاحِدَةٌ فَقَالَ أَكْفِلْنِيهَا وَعَزَّنِي فِي الْخِطَابِ ﴿٢٣﴾

24. Akasema: "Kweli amekudhulumu kwa kukuomba kondoo wako kuongeza katika kondoo wake; na bila shaka washirika wengi hudhulumiana wao kwa wao, isipokuwa wale walioamini na kutenda mema; na hao ni wachache." Na mara Daudi akaona ya kwamba tumemtia mtihanini (na ameanzuka). Akaomba maghufira kwa Mola wake, na akaanguka kunyenyekea na akaelekea (kwa Mola wake).

قَالَ لَقَدْ ظَلَمَكَ بِسُؤَالِ نَجَّتِكَ إِلَى نِعَاجِهِ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْخُلَطَاءِ لِيَبْغِيَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَقَلِيلٌ مَا هُمْ وَظَنَّ دَاوُدُ أَنَّمَا فَتَنَّاهُ فَاسْتَغْفَرَ رَبَّهُ وَخَرَّ رَاكِعًا وَأَنَابَ ﴿٢٤﴾

25. Basi tukamghufuria (tukamsamehe) hayo. Na kwa hakika ana yeye kwetu cheo kikubwa na mahali pazuri (marejeo mazuri).

فَغَفَّرْنَا لَهُ ذَلِكَ وَوَرَّانَا عَنْهُ تَالُوتَ وَحَسَنَ مَا بَ ﴿٢٥﴾

26. "Ewe Daudi! Hakika tumekujaalia kuwa Khalifa katika ardhi, basi wahukumu watu kwa haki wala usifuate matamania ya nafsi yasije yakakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa yakini wale wanaopotea, wakaacha njia ya Mwenyezi Mungu, wao watapata adhabu kali kwa sababu ya kusahau (kupuuza) kwao siku ya Hisabu."

يَا دَاوُدُ إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعِ الْهَوَى فَيُضِلَّكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّ الَّذِينَ يَضِلُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا نَسُوا الْحِسَابَ ﴿٢٦﴾

23-33. Makadiyani wamesema uwongo kwa kule kusema kuwa hao waliomjia Nabii Daudi si Malaika. Na yote haya ni kule kukataa kwao mambo ya Kiroho — Malaika na Majini na Mashetani na kama haya. Na vile vile katika Aya waliyoifanya ya 35 hawakusema kweli.

24. Kosa alilolifanya ni kule kukata hukumu kabla ya kusikiliza upande wa pili. Hizo Hadithi nyingine zinazotajwa katika baadhi ya vitabu vya tafsiri si sahihi hata kidogo. Haimkiniki kwa Mtume kumuashiki mke na mtu; kinyume cha zinavyosema Hadithi hizo.

27. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake bure. Hii ni dhana ya wale waliokufuru. Basi adhabu kali ya Moto itawathubutikia wale waliokufuru.

28. Je! Tuwajaalie wale walioamini na kutenda mema kuwa sawa na wafanyao uharibifu katika ardhi? Au tuwajaalie watawa (wacha Mungu) kuwa sawa na waovu? Hatufanyi sisi hivyo).

29. (Na hiki) Kitabu; tumekiteremsha kwako, chenye baraka nyingi; ili wapate kuzifikiri Aya zake, na wenye akili wawaidhike.

30. Na tukampa Daudi (mtoto anayelitwa) Suleimani, aliyekuwa mtu mwema; na alikuwa mnyenyekevu mno.

31. (Kumbukeni) alipopelekewa jioni farasi walio kimya wasimamapo, wepesi wakimbiapo.

32. Basi akasema: "Navipenda vitu vizuri kwa kumkumbuka Mola wangu." Kisha (mafarasi) wakafichikana nyuma ya kizuizi (kwa kutiwa zizini mwao. Nabii Suleimani akataka awaone tena akasema):

33. "Warudisheni kwangu," na akaanza kuwapangusa (kuwapapasa) miguu (yao) na shingo (zao).

34. Na tulimtia mihanini Suleimani na tukauweka mwili (mwengine) juu ya kiti chake, kisha akarejea (mwenyewe).

35. Akasema: "Mola wangu! Nisamehe na Unipe Ufalme, asiupate yoyote baada yangu (ya kunipa mimi mpaka niondoke ulimwenguni). Bila shaka wewe ndiwe Mpaji (Usiyenyima)."

36. Basi tukamtiushia upepo unaokwenda pole pole kwa amri yake, anakotaka kufika (unamfikisha. Na sasa sisi tumeonyesha kidogo haya kwa kupanda eropleni)

37. Pia na (tukamtiushia) mashetani, kila ajengaye na azamiaye (lulu)

38. Na wengine wafungwao minyororoni (wanapokhalifu amri zake).

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَاطِلًا  
ذَلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا: قَوْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا  
مِنَ النَّارِ ۝

أَمْ نَجْعَلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ  
كَالْمُقْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّقِينَ كَالْفُجَّارِ ۝

كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ مُبَارَكٌ لِيَدَّبَّرُوا آيَاتِهِ وَلِيَتَذَكَّرَ أُولُو  
الْأَلْبَابِ ۝

وَوَهَبْنَا لِدَاوُدَ سُلَيْمَانَ نِعَمَ الْعَبْدِ إِنَّهُ أَوَّابٌ ۝

إِذْ عَرَضَ عَلَيْهِ بِالْعِشِيِّ الصُّفُنَاتِ الْجِيَادِ ۝

فَقَالَ إِنِّي أَحْبَبْتُ حُبَّ الْخَيْرِ عَنْ ذِكْرِ رَبِّي ۝ حَتَّى  
تَوَارَتْ بِالْحِجَابِ ۝

رُدُّوهَا عَلَيَّ فَطَفِقَ مَسْحًا بِالسُّوقِ وَالْأَعْتَاقِ ۝

وَلَقَدْ فَتَنَّا سُلَيْمَانَ وَأَلْقَيْنَا عَلَى كُرْسِيِّهِ جَسَدًا  
ثُمَّ أَنَابَ ۝

قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَهَبْ لِي مُلْكًا لَّا يَنْبَغِي لِاحِدٍ مِّنْ  
بَعْدِي إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ ۝

فَسَخَّرْنَا لَهُ الرِّيحَ تَجْرِي بِأَمْرِهِ رُخَاءً حَيْثُ أَصَابَ ۝

وَالشَّيَاطِينَ كُلَّ بَنَّاءٍ وَعَوَّاصٍ ۝

وَالْآخِرِينَ مُمْتَرِينَ فِي الْأَصْفَادِ ۝

34. Ndugu yake Nabii Suleimani mkubwa wake, ambaye hakuwa Mtume wala mfalme, alimuonea maya (wivu) Nabii Suleimani; akazaititi vita akapigana naye na akashindwa Nabii Suleimani. Kisha Nabii Suleimani akamshinda barabara rdugu yake huyu.

39. (Tukamwambia:) “Hiki kipawa chetu (tulichokupa), (atia tuliyokupa) bila ya hisabu; basi toa uwape uwatacao au zuia; (khiari yako).”

40. Na kwa yakini ana yeye kwetu cheo (cha kukaribishwa kwetu), na mahali pazuri.

41. Na mkumbuke mja wetu Ayubu, alipomwita Mola wake, (akanena): “Kwa yakini Shetani amenifikishia udhia na taabu. (Niondoshee Mola wangu maradhi haya yaliyonishika).”

42. (Mwenyezi Mungu akamwambia):- “Uharikishe mguu wako (patachimbuka chechem chini yake, maji yake yatakuwa dawa yako). Basi haya maji baridi ya kuogea (koga), na (haya maji baridi) ya kunywa, (yanywe).”

43. Na tukampa watu wake na wengine kama wao pamoja nao, kwa rehema itokayo kwetu, na (ipate kuwa) mauidha kwa watu wenye akili.

44. “Na shika kicha cha vijiti tu mkononi mwako, (si fimbo); kisha mpige kwacho (mkeo kwa kiapo ulichoapa kuwa utampiga kwa mabaya aliyoyafanya), wala usivunje kiapo.” Bila shaka tulimkuta ni mwenye subira, mja mwema; kwa hakika alikuwa mnyenyekevu sana.

هَذَا عَطَاؤُنَا فَامْنُنْ أَوْ أَمْسِكْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ۝

وَأَنَّ لَهُ عِنْدَنَا لَزُلْفَىٰ وَحَسَنَ مَّآبٍ ۝

وَأَذْكُرْ عَبْدَنَا أَيُّوبَ ۖ إِذْ نَادَىٰ رَبَّهُ أَنِّي مَسَّنِيَ الشَّيْطَانُ  
بِنُصَبٍ وَعَذَابٍ ۝

أُرْكُضْ بِرِجْلِكَ هَذَا مُغْتَسَلٌ بَارِدٌ وَشَرَابٌ ۝

وَوَهَبْنَا لَهُ أَهْلَهُ وَمِثْلَهُم مَّعَهُمْ رَحْمَةً مِنَّا وَذِكْرًا  
لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ۝

وَخَذَ بِيَدِكَ ضِعْفًا فَاصْرَبْ بِهِ وَلَا تَحْتَسِبْ أَنَّا  
وَجَدْنَاهُ صَابِرًا نِعْمَ الْعَبْدُ إِنَّهُ أَوَّابٌ ۝

41. Makadiyani sharti wapindue muradi wa maneno ya Mwenyezi Mungu ili yasipatikane mamoo yanayokhusiana na roho. Wanageuza sheytan ndivyo hapa katika Aya hii waliyoifanya ya 42 kwa tafsiri nyingine, siyo ile waliyoifasiri katika *Shayaatyn* iliyoko katika Aya waliyoifanya ya 66 ya *Suratus Saaffaat*. Hapa wanasema *Sheytan* maana yake Kiu, na wanasema kuwa mwenye Qamus (Dictionary) ndivyo alivyofasiri hivyo. Waongo wakubwa! Mwenye Qamusi hakusema hivi. Yeye amesema *Sheytanut Taaq* maana yake . . . Na *Shaytanul Falaa* = Kiu. Hakusema kuwa tamko la *Sheytan* tupu huwa lina maana ya kiu. Waongo wakubwa. Na hata lugha yetu ya Kiswahili tuna matamko mengine, ambayo yakiwa peke yake huwa na maana nyingine na yakichanganyishwa na jina jingine huwa na maana nyingine.

Kwa mfano:-

(a) “Komba Mwiko:” Komba ni mnyama — wengine tunamjua. Na mwiko wengi pia tunaujua. Lakini likichanganyika tamko la Komba na Mwiko, ukasema “kombamwiko” inakuwa maana yake ni Mende huyu wa chooni na uchafuni. Wala hapana mnasaba baina yake na mwiko wala baina yake na komba.

(b) “Maziwa ya watu wawili:” Maziwa tunayajua, na watu tunawajua. Na hilo tamko la Maziwa ya Watu Wawili ni jina la dawa. Wala haifanywi kwa maziwa ya watu wawili.

(c) “Kozi Mwamba:” Tamko la Kozi tunalijua, na Mwamba wa bahari pia tunaujua au tunausia. Na yakichanganywa pamoja matamko haya huwa jina la ndege ambaye hakukhusika na kozi la mnazi wala mwamba wa bahari.

(d) “Mjomba Kaka:” Mjomba tunamjua, na Kaka pia tunamjua. Lakini yakichanganyishwa pamoja huwa ni yule mjusi anayeelekezwa fimbo na watoto ili arambe.

(e) “Kijumba Mshare:” Mshare na kijumba, yote tunayajua. Na yakichanganywa yanakuwa jina la ndege mdogo hivi.

Na yako mengi mengineyo.

Wala hakuna mfasiri yoyote aliyofasiri shaytan hapa wala kwingineko kuwa maana yake kiu kabla ya ukafiri wao huu.

44. Na wameupindua muradi wa tamko: *Wakhudh Biyadiha Dhighthan Fadhril Bihi* lililomo katika Aya waliyoifanya ni ya 45. Tafsiri yake ya haki itazame katika hii tafsiri yetu.

45. Na wakumbuke waja wetu (hawa):- Ibrahimu na Is-haka na Yaakubu waliokuwa wenye nguvu (katika mambo ya dini) na busara.

46. Hakika sisi tuliwachagua kwa lile jambo zuri kabisa la kuikumbuka Akhera.

47. Na bila shaka walikuwa mbele yetu (kwetu) ni miongoni mwa watu bora waliochaguliwa.

48. Na mkumbuke Ismaili na Alyasaa na Dhulkifli; na hao wote walikuwa miongoni mwa watu bora.

49. Huu ni ukumbusho (wa watu wema). Na kwa yakini wamchao Mungu mahali pao pa kurudia patakuwa pazuri kabisa

50. Mabustani ya kukaa milele yatakayofunguliwa milango (yake) kwa ajili yao.

51. Humo watagemea matakiani, wawe wanaagizia humo matunda mengi mengi (na mazuri), na vinywaji (vya kila namna).

52. Na pamoja nao (watakuwako) wake (zao) watulizao macho kwa waume zao, hirimu zao, (umri mmoja na wao). (Waambiwe:)

53. "Haya ndiyo yale mliyoahidiwa (kuyapata) siku ya kulipwa (viumbe)."

54. Hakika hiyo ndiyo riziki yetu (tutakayowapa), isiyomalizika, (isiyotindika).

55. Hivyo (ndivyo itakavyokuwa). Na kwa hakika wale warukao mipaka, pa kurudia pao patakuwa pabaya

56. Jahanamu — Wataingia. Nayo ni matengenezeo mabaya kabisa.

57. Ndivyo hivyo (itakavyokuwa). Basi waonje (wanywe) maji ya moto na usaha

58. Na (adhabu) nyingine za namna hii nyingi. (Kila likitiwa jeshi jengine huko Motoni waambiwe wale waliotangulia:

59. "Hili ndilo jeshi litakaloingia pamoja nanyi" (Wale wa zamani waseme): "Hawakupata mahala pazuri pa kufikia, hakika wao wanaingia Motoni."

60. Waseme (hawa wanaotiwa sasa kuwajibu): "Lakini nyinyi ndio (wa kuambiwa): hamna

وَأَذْكُرْ عَبْدَنَا إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ أُولَى الْأَيْبَى وَالْأَبْصَارِ ۝

إِنَّا أَخَصَّصْنَاهُمْ بِمَخَالِصَةٍ ذُكِّرْنَا فِي الدَّارِ ۝

وَاللَّهُمَّ عِنْدَنَا لِمَنِ الْمُصْطَفَيْنِ الْأَخْيَارِ ۝

وَأَذْكُرْ إِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَذَا الْكَيْفِ وَكُلَّ مِنَ الْأَخْيَارِ ۝

هَذَا ذِكْرُهُ وَإِنَّ لِلْمُتَّقِينَ لَحُسْنَ مَآبٍ ۝

جَدَّتْ عَدْنٌ مُفْتَحَةٌ لَهُمُ الْآبْوَابُ ۝

مُتَّكِبِينَ فِيهَا يَدْعُونَ فِيهَا بِفَاكِهَةٍ كَثِيرَةٍ

وَسَرَّابٍ ۝

وَعِنْدَهُمْ قَصْرٌ مَقْرِنٌ الْظَّرْفِ أُنْرَابٍ ۝

هَذَا مَا تُوْعَدُونَ يَوْمَ الْحِسَابِ ۝

الْبَابُ

إِنَّ هَذَا لِرِزْقِنَا مَا لَهُ مِنْ تَفَادٍ ۝

هَذَا وَإِنَّ لِلظَّالِمِينَ لَشَرَّ مَآبٍ ۝

جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا فَيَسَّرُ اللَّهُ لَهُمْ

هَذَا، فَلْيَذُوقُوا حَرِّ جَهَنَّمَ وَعَسَائِقُ ۝

وَأُخْرُونَ مِنْ شَكْلِهِ أَرْوَاجُ ۝

هَذَا قَوْمٌ مُفْتَحَتْ مَعَكَرُهُ لَأَمْرَجِبًا بِهِمْ، إِنَّهُمْ صَلَوُوا

النَّارِ ۝

قَالُوا بَلْ أَنْتُمْ لَا مَرْجَبًا بِكُمْ، أَنْتُمْ قَدَّمْتُمُوهُ

makaribisho mema! Nyinyi ndio mliotusabibishia adhabu. Mahala pabaya kabisa hapo.”

61. Waseme (waliokuja nyuma): “Mola wetu! Waliotusabibishia haya wazidishie adhabu mara mbili, (mara nyingi) huku Motoni.”

62. (Kisha wale wabaya wakishakuwa huko Motoni) watasema: “Imekuwaje! Mbona hatuwaoni wale watu tuliokuwa tukiwahisabu katika waovu (kwa kumfuata Muhammad)?”

63. “Je! Tuliwafanyia mzaha (huko duniani, na hali ya kuwa ni watu wakubwa Akhera au wamo Motoni humu pamoja na sisi) ila macho (yetu) haya waoni tu?”

64. Bila shaka haya ya kuhasimiana watu wa motoni — ni kweli.

65. Sema: “Hakika mimi ni Muonyaji tu; na hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, Mmoja, Mwenye nguvu.”

66. Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake, Mwenye nguvu, Mwingi wa msamaha.

67. Sema: “Haya (ninayokwambieni) ni habari kubwa kabisa ”

68. Mnajiepusha nayo (Mnaipuzza).

69. Sikuwa na ilimu ya mambo ya viumbe watukufu (Malaika) walipokuwa wakishindana, (ila amenijulisha Mwenyezi Mungu).

70. Haifunuliwi kwangu (kuambiwa) isipokuwa (kuambiwa hivi) kuwa mimi ni Muonyaji dhahiri.

71. (Kumbuka) Mola wako alipowaambia Malaika: Hakika mimi nitaumba mtu kwa udongo.

72. Na nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na mimi, basi mwangukieni kwa kumtii.

73. Basi Malaika wakatii wote pamoja.

74. Isipokuwa Ibilisi; alijivuna na akawa katika makafiri.

لَنَا فِي سَقَاتِ الْقَارِ ۝

قَالُوا رَبَّنَا مَنْ قَدَّمَ لَنَا هَذَا فَزِدْهُ عَذَابًا ضِعْفًا  
فِي النَّارِ ۝

وَقَالُوا مَا لَنَا لَا نَرَى رِجَالًا كُنَّا نَعْتَدُهُمْ وَمِن  
الْأَشْرَارِ ۝

أَتَعْتَدُ لَهُمْ سَعِيرًا ۝ لَمَّا رَأَتْ عَنْهُمْ الْأَبْصَارُ ۝

۝ إِنَّ ذَلِكَ لَحَقٌّ تَخَافُهُ أَهْلُ النَّارِ ۝

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ ۝ مُنذِرٌ وَمَأْسُومٌ ۝ وَإِلَّا اللَّهُ الْوَاحِدُ  
الْقَهَّارُ ۝

رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِينَ وَمَا بَيْنَهُمَا الْعَزِيزُ الْغَفَّارُ ۝

قُلْ هُوَ نَبِيُّ عَظِيمٍ ۝

أَتَنْتَهُرُ عَنْهُ مَعْرُضُونَ ۝

مَا كَانَ لِي مِنْ عِلْمٍ بِالْمَلَائِكَةِ إِذْ يَخْتَصِمُونَ ۝

إِنْ يَشَاءُ يُخَوِّئُنِي إِلَىٰ إِيَّاكَ ۝ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ ۝ مُبِينٌ ۝

إِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي خَالِقٌ بَشَرًا مِّنْ طِينٍ ۝

فَإِذَا سَوَّيْتَهُ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِي فَقَعُوا  
لَهُ سَاجِدِينَ ۝

فَسَجَدَ الْمَلَائِكَةُ كُلُّهُمْ أَجْمَعُونَ ۝

إِلَّا إِبْلِيسَ ۝ اسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ الْكَافِرِينَ ۝

72. Wamelipindua tamko la Ruuhy lililomo katika hii Aya waliyoifanya ni ya 73. Wala hapana mnasaba baina ya tamko la RUUHY lililoko hapa na tamko la RUUH (tupu si Ruuhy) lililopo katika hiyo Sura waliyoisema 40/16. Wanataka tu kudanganya. Ruuhy hii iliyopo hapa ni sawa sawa na Ruuhy iliyopo katika Aya ya 29 Suratul Hijr; na sawa sawa na Ruuhy iliyoko katika Aya ya 9 ya Suratul Sajda; na sawa sawa na Ruuhinaa zilizomo katika Aya ya 91 ya Suratul Anbiyaa na ya 12 iliyoko katika Suratut Tahrym. Na wao wanajua. Lakini basi tu wanapoteza.

Na watautia uwongo wao huu watakapofika katika Aya watakayoifanya ya 16 ya Suratul Muumin.

75. (Mwenyezi Mungu) akamwambia:- “Ewe Ibilisi! Kipi kilichokuzuia kumtii yule niliyemuumba kwa mikono yangu? Je! umetakabari, (wala huna ukubwa) au umo miongoni mwa wakubwa (kweli)?”

قَالَ يَا إِبْلِيسُ مَا مَنَعَكَ أَنْ تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِإِيْدِي  
أَسْتَكْبَرْتَ أَفَكُنْتَ مِنَ الْعَالِيْنَ ۝

76. Akasema: “Mimi ni bora kuliko yeye; kwani mimi umeniumba kwa moto, na yeye umemuumba kwa udongo.”

قَالَ أَنَا خَيْرٌ مِّنْهُ خَلَقْتَنِي مِنْ نَّارٍ وَخَلَقْتَهُ  
مِنْ طِينٍ ۝

77. (Mwenyezi Mungu) Akasema: “Basi toka humo kwani umebaidishwa na rehema.”

قَالَ فَآخِرٌ مِنْهَا فَأَنكَرَ رَجِيمٌ ۝

78. “Na hakika laana yangu itakuwa juu yako mpaka siku ya Malipo.”

وَأَنَّ عَلَيْكَ لَعْنَتِي إِلَى يَوْمِ الدِّينِ ۝

79. Akasema: “Mola wangu! Nipe nafasi (ya kuishi, nisife) mpaka siku watakayofufuliwa (viumbe).”

قَالَ رَبِّ فَأَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ ۝

80. (Mwenyezi Mungu) akamwambia: “Haya! Umekwisha kuwa miongoni mwa waliopewa nafasi (ya kuishi)”

قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِيْنَ ۝

81. “Mpaka wakati wa siku maalumu (ya kufa viumbe vyote, hapo na wewe utakufa).”

إِلَى يَوْمِ الْوَقْتِ الْمَعْلُومِ ۝

82. Akasema: “Na-apa kwa haki ya utukufu wako, bila shaka nitawapoteza wote (hao watoto wa huyu adui yangu—Adamu).”

قَالَ فِعْزَتِكَ لِأَعْوَابِهِمْ أَجْمَعِيْنَ ۝

83. “Isipokuwa wale waja wako miongoni mwao waliosafishwa (uliowasafisha).”

إِلَّا عِبَادَكَ وَنَهُمُ الْمُخْلَصِيْنَ ۝

84. Akasema (Mwenyezi Mungu) “Wallahi! Nasema kweli.”

قَالَ فَالْحَقُّ وَالْحَقَّ أَقُولُ ۝

85. “Kwa yakini nitaijaza Jahanamu kwa wewe na kwa hao wote wenye kukufuata miongoni mwao.”

لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنْكَ وَمِمَّنْ تَبَعَكَ مِنْهُمْ أَجْمَعِيْنَ ۝

86. Sema (Ewe Mtume kuwaambia watu wako): “Sikuombeni ujira juu ya haya (ninayokufundisheni); wala mimi si katika wale wanaojilazimisha (kufanya wasiyoyaweza. Hiyo ni sifa mbaya).”

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ وَمَا أَنَا مِنَ  
الْمُتَكَلِّفِيْنَ ۝


87. “Hayakuwa haya (ninayokwambieni) ila ni mauidha kwa walimwengu wote.”

إِنَّ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِيْنَ ۝

88. “Na bila shaka mtajua habari yake baadaye kidogo.”

يَعْلَمُ الْغُيُوبَ ۝

86. Uislamu haupendi mambo ya shida. Inataka katika kila unachokifanya ukifanye kwa kiasi cha mwisho wa ukomo wa uweza wako; ili kiwe kizuri na uweze kudumu nacho. Kudumu katika jambo lolote lile la kheri ndiyo bora, siyo leo kulifanya, kesho ukaliwacha. Na ukifanya lililopindukia mwisho wa ukomo wako, hutaweza kuendelea nalo; ima utachoka uliwache au utadhurika likuwache. Kawia Ufike, kuliko kulala njiani. Ukiwa huwezi kusimama, unapata ruhusa kusali kwa kukaa. Na ikiwa huwezi kufunga, unapewa ruhusa kufungua; khalafu ulipe. Na kama huwezi kuhiji basi huambiwi ukope wende ukahiji. Na mengineyo ni kama hivi.



Ina Aya 75

SURATUZ ZUMAR

Ina Makara 8

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Uteremsho wa Kitabu (hiki) umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ①

2. Kwa yakini sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa haki, basi muabudu Mwenyezi Mungu kwa kumfanya Mola yeye tu.

إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ فَاعْبُدِ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ ②

3. Wa kuitakidiwa Mola ni Mwenyezi Mungu tu; lakini wale wanaowafanya wengine kuwa waungu badala yake (husema:) "Sisi hatuwaabudu hawa ila wapate kutufikisha karibu kabisa na Mwenyezi Mungu." Hakika Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao katika yale wanayohitalifiana. Bila shaka Mwenyezi Mungu hamwongoi aliye muongo, aliye kafiri.

أَلَّا لِلَّهِ الدِّينَ الْخَالِصُ وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ فِي مَا هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ③ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ كَاذِبٌ كَفَّارٌ ④

4. Kama Mwenyezi Mungu angalitaka kupata mtoto bila shaka angalichagua amtakaye miongoni mwa aliowaumba. Lakini Yu mbali na hayo. Yeye ni Mwenyezi Mungu, Mmoja anayefanya atakayo.

لَوْ أَرَادَ اللَّهُ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا لَاصْطَفَىٰ مِمَّا يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ ۗ سُبْحٰنَهُ هُوَ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ⑤

5. Ameumba mbingu na ardhi kwa haki, hufunika usiku juu ya mchana, na hufunika mchana juu ya usiku. Na amelitiisha jua na mwezi; vyote vinakwenda tu (bila kusita) mpaka muda (wake) uliowekwa, jueni kwamba yeye (Mwenyezi Mungu) ni Mwenye nguvu, Mwingi wa kusamehe.

خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ بِالْحَقِّ ۗ يَكُوِّرُ اللَّيْلُ عَلَى النَّهَارِ وَيَكُوِّرُ النَّهَارُ عَلَى اللَّيْلِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۗ كُلٌّ يَجْرِي لِاَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ اَلَا هُوَ الْعَزِيزُ الْغَفَّارُ ⑥

6. Amekuumbeni katika nafsi moja, kisha akamfanya mwenziwe (mkewe) katika jinsi ile ile, na akakuteremshieni (akakuumbieni) wanyama wanane (hawa wenye nafuu kubwa kwenu) madume na majike. (Ngamia, Ng'ombe, Kondoo na Mbuzi).

خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَّاحِدَةٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَانزَلَ لَكُمْ مِنْ اَلْاَنْعَامِ ثَمَنِيَةَ اَزْوَاجٍ ۗ يَخْلُقْكُمْ فِي بُطُونِ اُمَّهَاتِكُمْ خَلْقًا مِّنْ بَعْدِ خَلْقٍ فِي ظُلُمٍ

3. Wa kuabudiwa na kuombwa ni Mwenyezi Mungu tu. Wala haitaki kuwaomba waliokufa ili wakufikishe kwake. Basi, dua inayoitwa *Wasyla*, haifai kuisoma, ni haramu. Tumeyasema sana haya mahala pengi.  
6. Viza vitatu: Kiza cha tumbo, kiza cha zalio na kiza cha mji, (ngozi inayomfunika).

Hukuumbeni matumboni mwa mama zenu — umbo baada ya umbo — katika viza vitatu. Huyu ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu: Ufalme ni wake; hakuna aabudwaye kwa haki ila yeye. Basi nyinyi mnageuzwa wapi?

7. Mkikufuru, basi Mwenyezi Mungu hana haja nanyi; lakini haridhii kufuru kwa waja wake; na kama mkishukuru, hayo yanamridhisha kwenu. Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine. (Kila mtu atateswa kwa dhambi zake). Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu. Basi atakwambieni yale mliyokuwa mkifanya. Bila shaka yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani (seuze yanayofanywa kwa viungo yakaonekana).

8. Na taabu inapomfika mtu humuomba Mola wake, akaelekea kwake. Kisha akimpa neema kutoka kwake, husahau yale aliyokuwa akimwitia zamani, na kumfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze (watu) na njia yake (Mwenyezi Mungu). Sema (kuwaambia hao makafiri):- “Starehe kwa kufuru yako muda kidogo tu kwani wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.”

9. Je, afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama na kuogopa Akhera na kutarajia rehema ya Mola wake (ni sawa na asiyefanya hayo)? Sema: “Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?” Wanaotanabahi ni wale wenye akili tu.

10. Sema: “Enyi waja wangu mlioamini! Mcheni Mola wenu. Wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema; na ardhi ya Mungu in wasaa. Na bila shaka wafanyao subira (wakajizuilia na maasia na wakaendelea kufanya ya taa) watapewa ujira wao pasipo hisabu.”

11. Sema: “Hakika nimeamrisha nimuabudu Mungu kwa kumuitakidi kuwa Mola ni yeye tu.”

12. “Na pia nimeamrisha niwe wa kwanza wa (viumbe) wanaojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu).”

13. Sema: “Mimi naogopa adhabu ya siku kubwa kama nikimuasi Mola wangu.”

14. Sema: “Namuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumuitakidi kuwa yeye tu ndiye Mwenyezi Mungu.”

15. “Basi nyinyi abuduni mnachopenda kisichokuwa yeye,” (khiari yenu, lakini Mwenyezi Mungu atakulipeni tu); Sema: “Hakika watakaopata

ثَلَاثًا ذِكْرُكُمْ لِلَّهِ رَبِّكُمْ لَهُ الْمَلَكُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَآلَئِكَ نُصَرِّفُوهٗنَّ ۝

إِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنْكُمْ وَلَا يَرْضَىٰ لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ وَإِنْ تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ مَرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ۝

وَلَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَا رَبَّهُ مُنِيبًا إِلَيْهِ ثُمَّ إِذَا خَوَّلَهُ نِعْمَةً مِّنْهُ نَسِيَ مَا كَانَ يَدْعُو إِلَيْهِ مِن قَبْلُ وَجَعَلَ لِلَّهِ أَنْدَادًا لِّبُضْلِهِ ۗ عَنِ سَبِيلِهِ قَاتِلُ تَمِيمٍ بِكُفْرِكَ قَلِيلًا ۗ إِنَّكَ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ ۝

أَمَّنْ هُوَ قَانِتٌ آنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذَرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُوا رَحْمَةَ رَبِّهِ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ۝

قُلْ يَعْبُدُ الَّذِينَ آمَنُوا لِقَاءَ رَبِّكُمْ ۗ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ ۗ وَأَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةٌ ۗ إِنَّمَا يُوَفَّى الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ۝

قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ ۝

وَأُمِرْتُ لِأَنْ أَكُونَ أَوَّلَ الْمُسْلِمِينَ ۝

قُلْ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ۝

قُلْ اللَّهُ أَعْبُدُ مُخْلِصًا لَهُ دِينِي ۝

فَاعْبُدُوا مَا شِئْتُمْ مِّن دُونِهِ ۗ قُلْ إِنَّ الْخَاسِرِينَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ وَأَهْلِيهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ

hasara ni wale waliozitia hasarani nafsi zaò na watu wao siku ya Kiama. Angalieni! Hiyo ndiyo hasara iliyo dhahiri.”

16. Yatawekwa juu yao mawingu ya Moto na chini yao mawingu (ya Moto vile vile). Kwa haya Mwenyezi Mungu anawaogopesha nayo waja wake. Enyi waja wangu! Niogopeni.

17. Na wale wanojepusha kufanya ibada ya masanamu, na wakanyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, habari njema (bishara njema) ni zao. Basi wape habari njema waja wangu hawa:

18. Ambao husikiliza kauli (nyingi zinazosemwa), wakafuata zile zilizo njema. Hao ndio aliowaongoa Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye akili.

19. Je, yule iliyemuajibikia hukumu ya adhabu (unaweza kumtengeneza)? Je! Unaweza kumuokoa aliyemo katika Moto?

20. Lakini waliomcha Mola wao watapata ghorofa zilizojengwa juu ya ghorofa; chini, (mbele) yake hupita mito. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu havunji ahadi (yake).

21. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mawinguni. Kisha akayapitisha (chini kwa chini), yakawa chemchem katika ardhi, tena akaotesha kwayo mimea ya rangi mbali mbali (na sura mbali mbali . . .)? Kisha hunyauka, ukaiona imekuwa kimanjano; kisha huifanya kukatikatika (ikapotelea mbali. Basi ndiyo ulimwengu unavyomuondokea mwenye nao) Bila shaka katika hayo muna ukumbusho kwa wenye akili.

22. Je! Mtu ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia (amemfungua) kifua chake kuukubali Uislamu, akawa yuko katika nuru itokayo kwa Mola wake (ni sawa na mwenye moyo mgumu)? Basi adhabu kali itawathubutikia wale wenye nyoyo ngumu wasimkumbuke Mwenyezi Mungu. Hao wamo katika upotofu (upotevu) uliyo dhahiri.

23. Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa (kwa kuteremsha) kitabu chenye maneno yanayowafikiana, (yasiyopingana) (na) yanayokaririwa (bila kuchosha); husisimka kwayo

الَّذِينَ هُوَ الْخَسِرَانِ الْمُبِينِ ۝

لَهُمْ مِنْ فَوْقِهِمْ ظُلْمٌ مِنَ النَّارِ وَمِنْ تَحْتِهِمْ ظُلْمٌ ذَلِكَ يُخَوِّفُ اللَّهُ بِهِ عِبَادَهُ لِيُعْبَادُوا فَاتَّقُوا ۝

وَالَّذِينَ اجْتَنَبُوا الطَّاغُوتَ أَنْ يَعْبُدُوهَا وَأَنَابُوا إِلَى اللَّهِ لَهُمُ الْبُشْرَىٰ، فَبَشِّرْ عِبَادِ ۝ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَاهُمُ اللَّهُ وَأُولَٰئِكَ هُمْ أُولُوا الْأَلْبَابِ ۝

أَفَمَنْ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ أَلَمْ يَأْتِ تَنْقِذًا مِنَ النَّارِ ۝

لَكِنَّ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ لَهُمْ غُرْفٌ مِمَّنْ فَوْقَهَا عُزْفٌ مُنْذِبَةً، يَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَعَدَّ اللَّهُ لَا يُخْلِفُ اللَّهُ الْمِيثَاقَ ۝

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَلَكَهُ يَنَابِيعٌ فِي الْأَرْضِ ثُمَّ يُخْرِجُ بِهِ زَرْعًا مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ ثُمَّ يَهَيِّجُ فَتْرَتَهُ مُمْفَرًا ثُمَّ يَجْعَلُهُ حُطَامًا إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرًا لَأُولِي الْأَلْبَابِ ۝

أَفَمَنْ شَرَحَ اللَّهُ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ فَهُوَ عَلَىٰ نُورٍ مِّنْ رَبِّهِ، قَوْلًا لِّلْقَيْبَةِ قُلُوبُهُمْ مِّنْ ذِكْرِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ فِي صُلْحٍ مُّبِينٍ ۝

اللَّهُ نَزَّلَ أَحْسَنَ الْحَدِيثِ كِتَابًا مُّتَشَابِهًا مَّثَانًا تَقْشَعُرُّ مِنْهُ جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ تَلِينُ

7. Rejca maelezo ya Aya ya 15 ya Bani Israil.

18. Inataka kwa mtu kusikiliza kila yanayosemwa, tena, afuate yale yaliyo mazuri.

23. Mwenyezi Mungu hamkalifishi mja wake, (hamtenzi nguvu) afuate anavyotaka yeye. Bali amempa huria

ngozi (miili) za wale wanaomwogopa Mola wao . . . Kisha ngozi zao na nyoyo zao huwa laini kwa kumkumbuka Mola wao. Huo ndio uwongofu wa Mwenyezi Mungu; kwa huo humuongoa amtakaye. Na anayeachiwa na Mwenyezi Mungu kuwa amepotea, basi hakuna wa kumuongoa.

24. Je! Yule atakayekuwa anaukinga uso wake na adhabu mbaya siku ya Kiama (ni sawa na yule atakayekuwa katika starehe za Peponi?). Na walio dhulumu wataambiwa: "Onjeni (jaza ya) yale mliyokuwa mkiyachuma."

25. Waliokuwa kabla yao walikadhibisha; na adhabu ikawajia kutoka mahali wasipopatambua.

26. Basi Mwenyezi Mungu akawaonjesha hizaya (fedheha) katika maisha ya dunia. Na adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi; laiti wanalijua!

27. Na bila shaka tumewapigia watu mifano ya kila namna katika hii Qurani ili wapate kukumbuka.

28. Qurani iliyoteremka kwa lugha ya Kiarabu (ifafanuyayo vizuri); isiyo na kombo (upotofu). (Wameteremshiwa hii Qurani) ili wajilinde (na kila mabaya).

29. Mwenyezi Mungu anakupigieni mfano wa mtu mwenye mabwana washirika wanaogombana, na wa mtu (mwingine) aliyehusika na bwana mmoja tu. Je! Wako sawa katika hali zao? Alhamdu lillahi, lakini wengi wao hawajui. (Basi shughulika na bwana wako mmoja tu Mwenyezi Mungu.)

30. Kwa yakini wewe utakufa na wao pia watakufa.

31. Kisha bila shaka mtashitakiana siku ya Kiama mbele ya Mola wenu.

جَلَدُوهُمْ وَقَلُوبُهُمْ إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ ذَٰلِكَ هُدَىٰ اللَّهِ  
يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ ۚ وَمَن يُضِلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ  
مِن هَادٍ ۝

أَفَمَن يَبْتغِي بِوَجْهِهِ سَوَاءَ الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ  
وَقِيلَ لِلظَّالِمِينَ ذُوقُوا مَا كُنتُمْ تَكْسِبُونَ ۝

كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ فَآتَهُمُ الْعَذَابُ مِن  
حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ۝

فَإِذَا قَامَ اللَّهُ الْآخِرَىٰ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَالْعَذَابُ  
الْآخِرَةُ أَكْبَرُ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ۝

وَلَقَدْ صَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِي هَٰذَا الْقُرْآنِ مِن كُلِّ  
مَثَلٍ لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ۝

قُرْآنًا عَرَبِيًّا غَيْرَ ذِي عِوَجٍ لَّعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ۝

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَّجُلًا فِيهِ شُرَكَاءُ  
مُتَشَكِّسُونَ ۚ وَرَجُلًا سَلَمًا لِّرَجُلٍ ۚ هَلْ يَسْتَوِينَ  
مَثَلًا ۚ الْحَمْدُ لِلَّهِ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ۝

إِنَّكَ مَيِّتٌ ۚ وَاللَّهُ مَيِّتُونَ ۝

تَوَارِكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ ۝

١٧٠

١٧١

— kama alivyosema mara nyingi katika Qurani — kama vile kusema kama ilivyo katika Aya ya 7-10 za *Surat Washshams*—kuwa *Wanafsin Wamaa Sawwaahaa* (= Na nafsi na alivyoitengeneza). *Faalhamahaa Fujuurahaa Wataqwaahaa* (= Akaiifahamisha yaliyo mabaya kwake na yaliyo mema). *Qad Afllaha Man Zakkaahaa* (= Basi amefuzu mwenye kuitakasa hiyo nafsi yake). *Waqad Khaaba Man Dassaahaa* (= Na ameharibikiwa mwenye kuiviza hiyo nafsi yake). Na akasema katika Aya ya 10 ya *Suratul Balad*:- *Wahadaynuahun Najdayn* (= Tukamwonyesha zote njia mbili — aifuata njema, ajiepushe na mbaya ili afuzu). Na akasema mara nyingi: *Famunshaa Falyuumin* (= Anayetaka naamini); *Wamanshaa Falyakfur* (= Na anayetaka naakufuru — kiuari yake, hapana kulazimishwa). Na akasema mahali pengi kuwa Yeye humsaidia anayetaka kusaidiwa, na humwachilia mbali asiyekubali kutengeneza. Amesema katika Aya ya 17 *Surat Muhammad*: *Walladhynahadaw Zaadahum Huda* (= Na wale waliokubali kuongoka aliwazidishia uwongofu). Na akasema katika Aya ya 86 ya *Suratu Aali Imran*:- *Kayfa Yahdillahu Qawman Kafaruu Baada Iymaanihim Washahiduu Annar Rasuula Haqqun Wajaahumul Bayyinaatu, Wallahu Laa Yahdil Oawmaadh Dhalimyn* (= Vipi atawaongoa Mwenyezi Mungu watu ambao wamekufuru baada ya Uislamu wao, na baada ya kushuhudia kwao kuwa Mtume huyu wa haki, na baada ya kuwajia hoja zote? Basi Mwenyezi Mungu hawagongoi watu wanaojidhulumu nafsi zao.)

32. Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na kuikadhibisha kweli imjiapo? Je, siyo katika Jahanamu makazi ya hao makafiri?

33. Na aliyeleta ukweli na aliyeusadikisha — hao ndio wamchao Mwenyezi Mungu.

34. Watapata watakachotaka kwa Mola wao; hayo ndiyo malipo ya watendao mema;

35. Ili Mwenyezi Mungu awafutie ubaya walioufanya na kuwalipa ujira wao kwa wema waliokuwa wakiutenda.

36. Je, Mwenyezi Mungu hamkifii (hamtoshei), mja wake? Na wanakuogofisha (wanakukhofisha) wale walio kinyume chake, (masanamu; kuwa watakudhuru kama hutawaabudu. Wanaweza wapi kudhuru, licha kunufaisha!). Na aliyehukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hana wa kumuongoa.

37. Na ambaye Mwenyezi Mungu anamuongoa hakuna awezaye kumpoteza, Je! Mwenyezi Mungu si Mwenye nguvu, anayeweza kulipa kisasi?

38. Na ukiwauliza: “Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi?” Bila shaka watasema: “Ni Mwenyezi Mungu.” Sema: “Je, Mnawaonaje wale mnaowaomba kinyume cha Mwenyezi Mungu, kama Mwenyezi Mungu akitaka kunidhuru, wao wanaweza kuniondolea dhara yake? au akitaka kunirehemu, je, wao wanaweza kuzuia rehema yake?” Sema: “Mwenyezi Mungu ananitoshia, kwake wategemea wanaotegemea ”

39. Sema: “Enyi watu wangu! Fanyeni amali zenu kwa tamkini yenu, (mpendavyo), mimi pia nafanya (kwa tamkini yangu). Basi karibuni hivi mtajua ”

40. “Ni nani itakayemjia adhabu ya kumfedhehesha na itakayemshukia adhabu iendeleayo.”

41. Sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa ajili ya watu (wote) ili kuwabainishia haki, basi anayeongoka (anaongoka) kwa manufaa ya nafsi yake, na anayepotoka bila shaka anapotoka kwa hasara (ya nafsi) yake pia. Na wewe siye mlinzi wao.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَبَ عَلَى اللَّهِ وَكَذَّبَ بِالصِّدْقِ إِذْ جَاءَهُ ۗ أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ ﴿٣٢﴾  
وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿٣٣﴾

لَهُمْ مَا يَشَاءُونَ عِندَ رَبِّهِمْ ۗ ذَٰلِكَ جَزَاؤُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٤﴾  
يُكَفِّرُ اللَّهُ عَنْهُمْ أَسْوَأَ الَّذِي عَمِلُوا وَيَجْزِيهِمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٣٥﴾

أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ ۗ وَيُخَوِّفُونَكَ بِالَّذِينَ مِنْ دُونِهِ ۗ وَمَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ﴿٣٦﴾

وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُضِلٍّ ۗ أَلَيْسَ اللَّهُ بِعَزِيزٍ ذِي انْتِقَامٍ ﴿٣٧﴾

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ  
اللَّهُ ۗ قُلْ أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرَادَنِيَ اللَّهُ بِضُرٍّ هَلْ هُنَّ كَافٍتٌ صُورُهُ أَوْ أَرَادَنِي بِرَحْمَةٍ هَلْ هُنَّ مُمْسِكَتٌ رَحْمَتِهِ ۗ قُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ عَلَيْهِ يَتَوَكَّلُ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٣٨﴾

قُلْ يَقَوْمِ اعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَامِلٌ ۗ سَوْفَ تَعْمَلُونَ ﴿٣٩﴾

مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ وَيَحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٤٠﴾

إِنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ لِلنَّاسِ بِالْحَقِّ ۗ فَمَنْ اهْتَدَىٰ فَلِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۗ وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ ﴿٤١﴾

36. Nawasikie wanaoomba makaburi na mizimu na . . . wakamuacha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hawezi kuwatosheliza? Na waisome vile vile Aya ya 38 na ya 43 na ya 44 na ya 45 za Sura hii hii. Wanataka waambiweje zaidi kuliko hivi?